SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Polepole** avuliwa uongozi Kamati ya Kudumu ya Bunge

UKURASA 2



**Irene** atamba kuvuka mipaka kutangaza injili

UKURASA 20

Nipashe
JUMAPILI
MWANGA WA JAMII
Jumapili Oktoba 10, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0580729
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Watumia vitabu kusafirisha 'unga'

UKURASA 3

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### MBUNGE AMPONGEZA SAMIA BAJETI BARABARA

MBUNGE wa Morogoro Mjini, AbdulAziz Abood, amempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuongeza bajeti ya kwa ajili...

UKURASA WA 3

### MAKAMBA ATETA NA BALOZI WA MAREKANI

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amekutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Marekani nchini, Donald Wright...

UKURASA WA 8

### USIRI SUMU KWA USTAWI WA NDOA

USIRI katika mambo ya fedha na mali huhatarisha uhai wa ndoa. Kukosekana kwa uwazi na uaminifu katika fedha...



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akikabidhi zawadi ya cheti kwa mwanafunzi asiyeona wa Shule ya Msingi Buhangija, mkoani Shinyanga, Faraja Robert, baada ya kuibuka mshindi wa kuandika barua, katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Posta Duniani, jijini Dodoma jana. Kushoto ni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Mpango alitaka Shirika la Posta kujitathmini

UKURASA 2

## RIPOTI MAALUM

### KINYESI CHA KUKU

# Lulu mpya katika ufugaji wa samaki na kilimo cha mboga

UKURASA 4 & 5

MICHEZO STARS KUPINDUA MEZA LEO BENIN UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# Polepole avuliwa uongozi kamati kudumu Bunge

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amefanya mabadiliko madogo ya wajumbe wa kamati za kudumu za Bunge kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni 2020.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Ofisi ya Bunge, mabadiliko hayo yanawagusa wabunge: Godwin Kunambi anayehamishwa kutoka Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwenda Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii na Humphrey Polepole anayehamishwa kutoka Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa kwenda Kamati ya Sheria Ndogo.

Kutokana na mabadiliko hayo, Polepole ambaye ni Mbunge wa Kuteuliwa, anapoteza nafasi aliyokuwa nayo ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa.

Mabadiliko yaliyofanywa na Spika Ndugai pia yamewagusa wabunge: Asia Halamga, aliyeteuliwa kuwa Mjumbe ya Kamati ya Masuala ya UKIMWI; Dk. Faustine Ndugulile aliyeteuliwa kuwa mjumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo na Kamati ya Masuala ya UKIMWI.

Aliyekuwa Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ameteuliwa kuwa mjumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo; aliyekuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamuriho, ameteuliwa kuwa mjumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo; na Agnes Marwa ameteuliwa kuwa mjumbe wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI.

# Mpango alitaka Shirika la Posta lijitathmini upya

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameltaka Shirika la Posta Tanzania kujitathimi na kuzifanyia kazi dosari mbalimbali zilizopo ili kuukabili ushindani wa soko katika sekta ya usafirishaji wa mizigo na vipeto uliopo hivi sasa duniani.

Dk. Mpango aliagiza hayo jana jijini Dodoma alipofunga maadhimisho ya Siku ya Posta Duniani.

"Hatuna budi kujitathmini kwa huduma zetu za Posta kama zinazingatia vigezo. Vilevile, tujipime vizuri kama huduma zetu zinaendana na maendeleo yaliyofikiwa na nchi yetu katika uchumi wa kati," alisema Dk. Mpango.

Alisema moja kati ya dosari ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi ni pamoja na matumizi ya fursa za kibiashara zilizopo nje ya nchi hasa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) pamoja na ile ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), ambazo bado hazijatumiwa vizuri na shirika hilo.

"Takwimu za huduma za Posta zinaonyesha kuwa huduma za Posta zinachangia chini ya asilimia 0.5 ya fedha za kigeni zitokanazo na mauzo ya huduma za Posta nje ya nchi huku tukiwa na fursa kubwa ya biashara katika jumuiya zetu,"alisema.

Dk. Mpango alilitaka shirika hilo kuongeza jitihada za kutangaza huduma zake ili jamii ipate kuelewa taswira mpya ya shirika nchini.

"Jana nilitembelea tovuti yenu, nikakuta iko katika lugha ya Kiingereza. Nani atawaelewa? Ninawaagiza sasa muweke pia katika lugha ya Kiswahili ili Watanzania wengi wapate kutambua huduma mnazozitoa," aliagiza.

Dk. Mpango pia alisema hivi sasa huduma za Posta zinakabiliwa na ushindani mkubwa, hivyo ili ziendele kuwa endelevu, ipo haja ya kuwapo kwa ubunifu.

"Ili huduma hizi ziendelee kuwa endelevu kuna haja ya kuwa wabunifu na kukidhi mahitaji ya wateja, ni lazima twende sawa na mabadiliko ya TEHAMA na mahitaji ya sasa ya dunia yanataka nini," alisema.

Kiongozi huyo wa serikali alibainisha kuwa kwa mujibu wa utafiti wa Benki ya Dunia (WB) wa mwaka 2004, ukuaji wa huduma za Posta unachochea ukuaji wa pato la mtu mmoja mmoja.

"Huduma za Posta zinatakiwa kuwa za uhakika ili kujenga imani kwa wateja, ikiwa ni pamoja na kuzingatia muda, usalama wa vitu vinavyotumwa. Pili, huduma zitolewe kwa ufanisi, kwa gharama nafuu na ubora wa hali ya juu"alisisitiza.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji, alisema mashirika ya Posta duniani yamewekeza katika teknolojia wakati huu ambapo dunia inakabiliwa na janga la UVIKO-19.

Katika maadhimisho hayo, Dk. Mpango alikabidhi vitendea kazi vya magari na pikipiki kwa Shirika la Posta Tanzania ili kuliwezesha kuongeza ufanizi katika utekelezaji wa majukumu yake mbalimbali.




Bajaj ikiwa imebanwa na daladala wakati dereva wake akitaka kupenya katika kituo cha Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dozi chanjo ya corona mbioni kumalizika Dar es Salaam

**Na Mary Geofrey**

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, amesema chanjo 160,000 walizopewa aina ya Johnson & Johnson ziko mbioni kumalizika baada ya kuongezeka kwa mwamko wa uhitaji wa huduma hiyo.

Aliyataja mambo yaliyochangia wakazi wa mkoa huo kuchangamkia chanjo hizo kuwa ni huduma ya mkoba ya nyumba kwa nyumba, kuongezeka kwa vituo vya kutolea chanjo kutoka 28 hadi 318 na elimu inayoendelea kutolewa na vyombo vya habari. Dk. Mfaume aliyaeleza hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya Siku ya Tiba Shufaa Duniani yenye kaulimbiu inayosema 'usimuache yeyote nyuma, usawa katika utoaji wa huduma za tiba shufaa.

Alisema uhitaji wa chanjo kwa wakazi wa mkoa huo ni mkubwa, hali ambayo inatia moyo kwa wataalamu wa afya kuona kuna mwamko mkubwa tofauti na siku za awali. "Kati ya chanjo 160,000 tulizopewa mkoa wetu, zilizobaki ni kidogo sana na wiki hii tunatarajia kuzimalizia na tutaendelea kutoa huduma kwa sababu kuna chanjo nyingine serikali imezipokea jana (juzi) kutoka kwa marafiki zetu, Serikali ya China," alisema Dk. Mfaume. Akizungumzia Tiba Shufaa, alisema ni asilimia 14 ya wagonjwa waliofikiwa na huduma hiyo kati ya wagonjwa wengi wanaostahili kuipata, kunakosababishwa na uhaba wa watoa huduma.

Aliwataka viongozi wa dini waendelee kushirikishwa kikamilifu katika kutoa Tiba Shufaa kwa sababu wana mchango mkubwa katika kuponya kwa njia ya imani.

Alisema pia kuongeza uelewa kwa kundi la watoa huduma na kupeleka taarifa kwa jamii kuhusu matumizi Tiba Shufaa ili jamii iwe na uelewa mpana katika kusaidia upatikanaji wa huduma hiyo.

Dk. Mfaume alisema Mkoa wa Dar es Salaam watatoa elimu kuhusu Tiba Shufaa kwa lugha rahisi na kuwafikia wananchi wengi katika kurahisisha upatikanaji wake.

Meneja Mpango wa Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Omary Ubuguyu, alisema wamekutana kwa ajili ya kupitia mwongozo na sera za Tiba Shufaa kwa sababu wameona kuna uhitaji mkubwa wa kuupitia na kufanya maboresho.

Alisema wanatakiwa kujenga hamasa kuhusu huduma za Tiba Shufaa zinazotolewa nchini na wanajamii, wataalamu wa afya na viongozi wa dini ili itolewe sambamba na tiba nyingine.

Alisema kundi kubwa la wagonjwa wanaotakiwa kupatiwa Tiba Shufaa halijafikiwa kwa sababu kati ya watu milioni tisa wanaougua magonjwa yasiyo ya kuambukiza, ni watu milioni tatu hadi tano wanaopata huduma hiyo.

**HABARI KITAIFA**

# Makamba ateta na Balozi wa Marekani

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amekutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Marekani nchini, Donald Wright pamoja na Balozi wa Uholanzi, Wiebe De Boer, akitaja vipaumbele katika sekta ya nishati.

Mazungumzo yake na mabalozi hao yalifanyika juzi katika Ofisi ndogo za Wizara ya Nishati mkoani Dar es Salaam na kuhudhuriwa na watendaji mbalimbali, akiwamo Kamishna wa Umeme na Nishati na Jadidifu, Felchesmi Mramba, Kamishna wa Petroli na Gesi, Michael Mjinja, na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC), Dk. James Mataragio.

Katika kikao chake na Balozi wa Marekani, Waziri Makamba alimweleza balozi huyo vipaumbele mbalimbali vya serikali katika sekta ya nishati ikiwamo upatikanaji wa umeme hasa katika maeneo ya vijijini.

Alisema serikali imefanya kazi kubwa ya kupeleka umeme maeneo hayo lakini wananchi wengi bado wanahitaji huduma hiyo. Waziri huyo alitaja kipaumbele kingine kuwa ni uwapo wa nishati endelevu za kupikia mfano gesi ya kwenye mitungi (LPG) ambayo itawafanya wananchi wengi waache kutumia mkaa na kuni kwa kupikia na hivyo kuondoa suala la uharibifu wa misitu ambalo pia linapelekea mabadiliko ya tabianchi.

"Kipaumbele kingine ni kuzifanya taasisi zilizo chini ya wizara kama vile TANESCO, TPDC na EWURA kuwa na uwezo wa rasilimali watu pamoja na uwezo wa kifedha utakaoziwezesha kuwa na ufanisi pamoja na usimamizi madhubuti wa sekta ya nishati hasa katika kipindi ambacho Tanzania inakwenda kuwa nchi yenye umeme wa kutosha katika ukanda huu," alisema Makamba.

Balozi wa Marekani, Wright, alisema ataendelea kufanya kazi na wizara na kwamba kumekuwa na ushirikiano wa takriban miaka 60 kati ya Tanzania na nchi hiyo na eneo mojawapo la ushirikiano huo ni sekta ya nishati.

Katika mazungumzo yake na Balozi wa Uholanzi nchini, Waziri Makamba alitaja maeneo mbalimbali yanayohitaji ushirikiano, kubwa ikiwa ni kupeleka umeme katika maeneo ambayo hayajafikiwa na umeme wa gridi kama vile visiwani kwa kuweka mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali ikiwamo jua ambalo linapatikana katika maeneo yote ya Tanzania.

Aliishukuru Uholanzi kwa kuwa na ushirikiano mzuri na Tanzania kwa miaka mingi na kwamba ushirikiano wa nchi hizo mbili upo katika sekta mbalimbali ikiwamo nishati.

Balozi wa Uholanzi, De Boer, alimweleza waziri huyo kuwa serikali isisite kuwasiliana na ubalozi huo pale inapoona kuna uhitaji wa kuungwa mkono katika utekelezaji wa mipango mbalimbali.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, ACP Stella Mutabihirwa akionyesha kwa waandishi wa habari jana, jinsi gramu 728.5 za dawa za kulevya aina ya Heroine, zilivyohifadhiwa ndani ya kurasa za vitabu vitatu tofauti, ambapo jeshi hilo, linamshikilia mtuhumiwa msichana Dorin Finan Lawrance (22), mkazi wa Tabata jijini Dar es Salaam, huku mwanamume aliyekuwa naye anayedaiwa kuwa ni raia wa nchi jirani, akifanikiwa kutoroka. **PICHA: ELISANTE JOHN**

# Vitabu vyatumika kusafirisha 'unga'

**Na Elisante John,** SINGIDA

JESHI la Polisi Mkoa wa Singida limebaini mbinu mpya ya kusafirisha dawa za kulevya, maarufu unga, wahusika wakidaiwa kutumia njia ya vifungashio kwa kuchana kurasa za vitabu kisha kugandisha upya kwa kutumia gundi na kuweka dawa katikati ya kurasa mbili.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Stella Mutabihirwa, alibainisha hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kumkamata Dorin Finan Lawrance, mkazi wa Tabata jijini Dar es Salaam, akidaiwa kusafirisha dawa ya Heroine gram 728.5 kwenda nchi jirani.

Alidai kuwa mtuhumiwa alifika katika ofisi za kampuni ya usafirishaji ya DHL eneo la stendi ya zamani mjini Singida, akiwa ameongozana na mpenzi wake, raia wa Kenya, lakini baadaye mpenzi wake huyo alikimbia baada ya kubaini hatari ya kukamatwa. Mutabihirwa alifafanua kuwa njia hiyo mpya siyo rahisi kuibaini kwa jinsi dawa hizo zinavyohifadhiwa kwa ustadi mkubwa ndani ya kurasa za vitabu vitatu kutokana na kuchana kurasa, kisha dawa kufungwa ndani kwa utaalamu wa hali ya juu.

Kamanda Mutabihirwa alisema kabla ya kufikia hatua ya kuandika anuani, mmoja wa maofisa wa Kampuni ya DHL aliushtukia mzigo huo, hivyo akahitaji ufunguliwe kwanza kwa uhakiki zaidi na mvutano ulianza na mtuhumiwa mmoja wa kiume aliamua kukimbia.

Alisema msako mkali unaendelea kumtafuta mtuhumiwa huyo afikishwe kwenye vyombo vya sheria kujibu tuhuma dhidi yake.

Katika tukio lingine, Kamanda Mutabihirwa alisema jeshi hilo linamshikilia Magidu Jisusi (55), mkazi wa Kijiji cha Mlandala, Kata ya Urughu wilayani Iramba kwa tuhuma za mauaji dhidi ya mtoto wake, Nchimwa Magidu (22), anayedaiwa kumshambulia kwa fimbo hadi kumsababishia kifo. Chanzo cha mauaji hayo kinadaiwa kuwa Magidu kwenda katika sherehe za jamii ya kisukuma na kujichagulia msichana kwa utamaduni wa kabila hilo wa 'chagulaga', lakini mzazi huyo hakufurahia hatua hiyo kutokana na kudaiwa mahari kubwa ya ng'ombe.

Kutokana na kutofurahishwa na kitendo hicho, mzazi huyo anadaiwa alipomtaka mwanawe amruhusu msichana kurejea kwao, aligoma.

"Kweli hii tabia ni mbaya na haifai katika jamii, kumpiga na fimbo binadamu mwenzako kwenye sehemu mbalimbali za mwili, tena anayempiga ni baba yake mzazi, huu ni ukatili na ninawaomba wananchi wa Singida waachane na vitendo vya kujichukulia sheria mkononi," alisema Mutabihirwa.

# Mbunge ampongeza Samia kuongeza bajeti ya barabara

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MBUNGE wa Morogoro Mjini, AbdulAziz Abood, ampongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuongeza bajeti ya kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya barabara katika Mkoa wa Morogoro kutoka Sh. bilioni 24.8 hadi Sh. bilioni 26.02 mwaka huu wa fedha.

Abood alitoa pongezi hizo wakati wa kikao cha 37 cha Bodi ya Barabara ya mkoa huo kilichofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Chuo cha Ualimu Morogoro.

Akizungumza katika kikao hicho, Abood alisema ongezeko la bajeti hiyo litasaidia kumaliza kero za miundombinu ya barabara katika Manispaa ya Morogoro na kufungua barabara zingine za pembezoni.

"Bado tuna matatizo ya miundombinu ya barabara katika Manispaa yetu ya Morogoro hasa katika barabara za mitaa, hivyo tunamshukuru Rais Samia kwa kutuongezea fedha za barabara katika bajeti, itasaidia kukarabati na kufungua barabara mpya," alisifu Abood.

Mbunge huyo alihaidi katika kikao hicho kuwa atakapokuwa bungeni, atahakikisha anasimamia upatikanaji wa fedha hizo kwa haraka ili kusaidia kukarabati miundombinu hiyo ambayo kwenye baadhi ya mitaa imekuwa kero kwa wananchi.

Mbunge wa Mikumi, Dennis Londo, akichangia katika kikao hicho, alisema kitendo cha Rais Samia kuongezea Mkoa wa Morogoro fedha za miundombinu, kimeonyesha dhahiri ana dhamira ya kuinua uchumi wa mkoa huo na nchi kwa ujumla.

Londo alisema fedha hizo pia zitaweza kusaidia kukarabati na kufungua barabara zilizopo katika Jimbo la Mikumi ambazo nyingine kwa muda mrefu zimekuwa zikipitika kwa shida na kuleta usumbufu kwa wananchi.

Awali, akifungua kikao hicho, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, alisema Serikali chini ya Rais Samia imeongeza fedha hizo ili kuimarisha miundombinu ya barabara, ikiwa ni njia bora ya kuinua uchumi wa mkoa huo.

Shigella alisema licha ya serikali kuongeza bajeti hiyo, kuna haja wabunge wa mkoa huo kusaidia upatikanaji wa fedha za kutosha za maendeleo kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wa miundombinu hususani ya barabara.

"Katika kikao hiki niwaombe waheshimiwa wabunge wetu wa Mkoa wa Morogoro kupaza sauti bungeni ili zipatikane fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara, ikiwamo ya Bigwa-Kisaki inayoelekea Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na kwenye bwawa la kuzalisha umeme wa MW 2, 115," alisema.

Alibainisha kuwa ongezeko hilo la bajeti linajumuisha fedha maendeleo kutoka Sh. bilioni 2.75 ya mwaka wa fedha 2020/21 hadi Sh. bilioni 5.37 mwaka huu wa fedha.

Shigella alisema serikali pia imetoa Sh. bilioni 2.4 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Bigwa-Kiroka kipande chenye urefu wa Km 15 kwa kiwango cha lami.

Uongozi wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) ulibainisha kuwa bajeti ya maendeleo ya mwaka wa fedha 2020/21 ilikuwa Sh. milioni 400 na bajeti ya mwaka 2021/22 imeongezeka hadi kufikia Sh. bilioni 23.93.

Shigella alisema matengenezo ya barabara katika mwaka wa fedha 20/2021 yalitengewa Sh. bilioni 8.07 na mwaka huu yameongezewa bajeti kufikia Sh. bilioni 8.23.

RIPOTI MAALUM

# KINYESI CHA KUKU

# Lulu mpya katika ufugaji wa samaki na kilimo cha mboga

## ■Mnufaika: Nina gari na nyumba za kisasa kwa wake zangu wote...



Mjasiriamali Christopher Mwita (kulia) akiwa kazini na vijana wake.

**Na Sanula Athanas**

UNAPOKANYAGA Mtaa wa Kiebikiri ulioko Kata ya Turwa wilayani Tarime mkoani Mara, katika orodha ya wajasiriamali wake, hakosekani Christopher Mwita mwenye umri wa miaka 48.

Mahali hapo ni umbali wa Km 4.3 kusini mashariki mwa Mji wa Tarime na safari yake kutoka mjini ni mwelekeo wa kufuata barabara ya lami ya Nyamwaga, kisha unachepuka kushoto ukipita kwenye barabara ya vumbi umbali wa mita 400 kulifikia shamba lake kutoka Shule ya Sekondari Mwera Vision inapoanzia barabara hiyo ya vumbi.

Kwa mbali anaonekana Mwita akiwa katika harakati za kuhudumia mifugo yake kwenye eneo ambalo maji yake ni ya chemchemi.

Uso wake umejawa tabasamu lenye mzizi wa mafanikio aliyoanza kuyashuhudia miaka 14 iliyopita katika shughuli zake za ufugaji mseto unaojumuisha kuku, samaki na bustani ya migomba na mboga (mchicha, sukumawiki, chinese na kunde).

Kinachoshuhudiwa katika mradi wake huo ni ujasiriamali usiozoeleka kwa wengi, kuku, samaki na bustani vinaendeshwa kwa wakati mmoja, eneo moja, vinategemeana na kila kimoja kikiwa na mazao maradufu ya kawaida.

Leo hii maisha ya Mwita, ambaye awali alikuwa akiendesha uzalishaji wa bidhaa hizo kienyeji, baadaye akapata darasa na kuthubutu kujitosa kwenye teknolojia hiyo mpya, yamekuwa yenye kicheko cha kudumu.

Uzalishaji wa samaki na kuku sasa umemwongezea theluthi mbili ya ilivyokuwa awali. Jicho zaidi likizama kwenye uchumi huo penye ubia wa samaki na bustani, penyewe pametikisa zaidi pakiwa na ongezeko linalokita asilimia 300.

Maisha yake kwa ujumla si haba. Pato lake kwa mwaka lina wastani wa mara mbili ya alivyokuwa zamani, huku akijidai kwa miliki ya nyumba mbili mpya, kila mama mtoto na yake, mwenyewe akizunguka hapa na pale akiwa ameshikilia usukani na kupiga honi mitaani, jambo ambalo awali lilikuwa tamthilia isiyo na ushuhuda halisi kwake.

### YAMEWEZEKANAJE HAYO?

Mjasiriamali Mwita anasimulia kwamba ni matokeo ya kile alichokianza mwaka 2004, lakini sura kubwa ya mafanikio ilijitokeza mwaka 2007 baada ya kupata darasa lililojitosheleza na kuibua majibu chanya yaliyoangukia hata kubadili haiba ya maisha yake ya kawaida.

Hiyo ilianza pale Mwita alipokuwa mnufaika wa mafunzo maalum ya ubunifu kutoka Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), hata yakamwezesha kupanua ufugaji wake kwa haraka pale mwaka 2004 yalipomwondoa kutoka kwenye ufugaji wa kienyeji, akiwa na bwawa la samaki lenye ukubwa wa mita za mraba 30 (mita tano kwa sita) na ndani ya mwaka mmoja akapanua kufikia mita za mraba 120 (mita 10 kwa 12), ambazo ni mara nne ya awali.

Mwita mwenye wake wawili na watoto sita (watatu wa kike), anasema alizidi kusonga mbele, akiainisha kutoka mwaka 2005 alipojitanua zaidi hadi kufikia bwawa lenye ukubwa wa mita za mraba 380 (mita 19 kwa 20). Hatua hiyo ya upanuzi wa mradi wa mabwawa, aliifanya kwa mtindo tofauti kidogo wa kuongeza mabwawa mengine mawili mapya, kila moja likiwa ni kubwa zaidi kuliko ya awali.

Anafafanua hali ya mabwawa hayo kwamba moja lina ukubwa wa mita za mraba 400 (mita 20 kwa 20) na lingine lenye ukubwa wa mita za mraba 450 (mira 15 kwa 30), ambayo kwa ujumla wake yameunda tafsiri mpya ya mafanikio yake kwenye ujasiriamali huo, yakiwa na muundo na mfumo wa uzalishaji mpya.

### UNAVYOENDESHWA

Kuhusu namna ya uzalishaji anaouendesha, Mwita anasema: "Kinachofanyika hapa unakuwa na bwawa la samaki, juu yake unajenga banda la kuku na pembeni ya bwawa unakuwa na bustani. Kinyesi cha kuku kikidondoka kwenye maji, kinakuwa chakula adhimu kwa ajili ya ukuaji wa samaki. Maji nayo yanapata rutuba inayomwagiliwa kwenye bustani.

"Muhimu hapo, hakikisha banda lako la kuku halisogei sana kwenye maji, walau mita moja na nusu au mbili kutoka kwenye maji maana usiku kunakuwa na baridi sana kwenye bwawa. Kuku wakipigwa na baridi kali, wanakonda. Wakikumbwa na hali hiyo, hutapata mayai. Pia ni muhimu kuweka uzio kuzungushia bwawa kwa ajili ya usalama wa samaki na kuku.

"Wakati ninaanza ufugaji mseto mwaka 2004, baadhi ya majirani waliniona kama nimepatwa na kichaa, lakini baada ya mafanikio wamekuwa miongoni mwa watu wengi wanaofika hapa kuja kujifunza na hata kununua kuku, samaki, mboga na ndizi.

"Nimekuwa nikipata wageni wanaokuja kujifunza kutoka mikoa ya Tabora, Arusha, Shinyanga, Dar es Salaam, Pwani, Mbeya na hata wanaotoka Uganda, na nimeitwa maeneo mengi kwenda kutoa elimu hii.

"Kwa kifupi, huu ni ufugaji wa gharama nafuu sana. Ninalisha kuku, kuku wanalisha samaki! Maji haya yenye rutuba yanatumika kumwagilia bustani, mazao ya bustani nayo yanakuwa chakula kwa hao wawili (kuku na samaki) na vyote hivyo unaweza kuvuna na kuuza. Shughuli inajiendesha yenyewe bila ya gharama kubwa.

"Wateja wangu ni wa hapa hapa Tarime, huwa ninauza bidhaa hapa hapa shambani kwangu. Wanunuzi wa jumla wa samaki na kuku huwa wanakuja ninawauzia, wao wanakwenda kuuza huko wanakojua."

Ndani ya falsafa ya kila mafanikio kuna magumu yake, hilo pia linajitokeza kwenye uzalishaji huo ambao Mwita anautolea ufafanuzi:

"Kikwazo katika mradi huu kwa sasa ni kwenye upatikanaji wa mbegu. Vifaranga vya samaki vinapatikana Arusha, Kenya na Uganda. Pia kunapokuwa na ukame, wale 'ndege mwarabu' wanakuja kwa ajili ya kusaka chakula, wanatua kwenye bwawa na kuchukua samaki.

"Kunapokuwapo kenge pia ni tatizo. Kuna shida ya vyura na nyoka, kunapokuwa na vyura ndani

INAENDELEA UK. 5



Bustani ya mjasiriamali huyo inayotumia maji ya ufugaji mseto.



Mwonekano wa mradi wa ufugaji mseto unaofanywa na mjasiriamali huyo mjini Tarime. **PICHA ZOTE: SANULA ATHANAS**

RIPOTI MAALUM

# Lulu mpya katika ufugaji wa samaki na kilimo cha mboga

INATOKA UK. 4

ya bwawa, lazima nyoka utawakuta, vinginevyo uweke samaki aina ya kambale, lakini sisi tunafuga zaidi samaki jamii ya sato.

"Usumbufu wa nyoka uko kwenye bwawa, wanaingia kwa ajili ya kula vyura. Ukipanda mchaichai kuzunguka bwawa, nyoka haingii. Pia tunatumia mbinu ya kuweka bata wadogo kwenye bwawa, kamwe nyoka haingii kwenye bwawa lenye bata hao."

Mjasiriamali Mwita bado anajifariji kwa madhila ya magumu hayo ndani ya ufugaji, akigeuzia shingo kwenye ulingo wa majumuisho ya mafanikio yake anayoyawasilisha kwa lugha ya tabasamu kwamba:

"Nilianza mradi huu nikiwa na mtaji wa Sh. 15,000 tu. Sasa nina uhakika wa kusomesha watoto wangu wote sita (mmoja yuko chuo kikuu na wengine wanasoma sekondari binafsi) na nimejenga nyumba za kisasa kwenye miji yangu miwili (wake wawili)."

Mwita ambaye kielimu aliishia elimu ya msingi, anabainisha kuwa wakati anaanza ufugaji wa samaki kwa njia ya kawaida mwaka 2004, alikuwa anapata faida ya Sh. milioni 2.5 kwa mwaka, lakini sasa kwenye ufugaji mseto anavuna faida ya Sh. milioni sita kwa mwaka, sawa na ongezeko la zaidi ya mara mbili.



Sehemu ya mafanikio ya Christopher Mwita katika ufugaji mseto wa samaki, kuku na bustani.

**THAMANI YA KINYESI**

Katika hali ya kawaida, sifa ya kinyesi cha wadudu na mifugo huangukia katika kurutubisha udongo. Lakini wanazuoni wataaluma husika wanasonga zaidi ya hapo, wakiangaza lishe kwa samaki, kurutubisha maji na yanayofanana nayo.

"Ndege wanakula vitu vingi vyenye rutuba lakini kiasili miili yao haina uwezo wa kufyonza virutubisho vyote, hivyo vinapodondoka kwenye bwawa vinakuwa na manufaa makubwa kwa ukuaji wa samaki," anafafanua Dk. Amon Shoko, Mtafiti kutoka TAFIRI.

Mbobezi mwenzake, Musa Ngematwa, aliyezama katika stadi ya ufugaji samaki, anaenda mahususi kwenye kinyesi cha kuku, akibainisha kuwa mbali na kuwa chanzo cha mbolea kilichozoeleka, pia kinaangukia kwenye urutubishaji wa bwawa la samaki, hasa panapofanyika ufugaji mseto baina ya pande hizo mbili zikitegemeana.

Ngematwa anasema ili kupata chakula cha asili kwa samaki ndani ya ufugaji huo mseto, kinyesi cha kuku hufanywa chanzo cha mbolea kwa sababu huwa kina kiasi kikubwa cha virutubisho vya urea, ambavyo vinahitajiwa kwa samaki kama lishe na mchango muhimu kwa afya yao.

Namna kinavyotumika, mtaalamu huyo wa mifugo anabainisha kwamba ni ama kinaliwa moja kwa moja na samaki pindi kinapodondoshwa bwawani au huwa chanzo cha rutuba kwenye bwawa lao.

"Hiki huwapa samaki afya nzuri kwani huwa na chembechembe nyingi za urea ambazo ni sehemu kubwa ya madini ya Naitrojeni na Fosforasi, ambayo huhitajika kwa wingi kwenye chakula cha samaki," anafafanua.

Lingine analolitaja mtaalamu huyo, ni kwamba mfugaji anapotumia utajiri wa kazi yake kama lishe, moja kwa moja anavuna manufaa mengi kiafya kutokana na viini lishe vya protini vinavyopatikana kwa mlo wa kuku, mayai, samaki na mboga, vyote vinapatikana kutoka mzunguko wa ufugaji huo tajwa.

Pia anadokeza katika eneo la uchumi kilimo kwamba ni aina ya ufugaji inayobeba chanzo cha pesa kama ilivyoshuhudiwa kwa mfugaji Mwita, na kuna pato la kutosha kukidhi mahitaji mengine ya maendeleo binafsi kutoka kwenye kila kilichofanyika ndani ya ufugaji huo.

Mtaalamu Ngematwa anahitimisha uchambuzi wake wenye wajihi wa afya na uchumi katika eneo hilo la ufugaji na kilimo, akipigia debe ufugaji huo wa kuku na mseto wake uliotajwa, kwamba unafanyika kirahisi na wa gharama nafuu kulinganisha na wanyama wakubwa kama ng'ombe, nguruwe, mbuzi na kondoo ambao wana kawaida ya kuhitaji mitaji mikubwa na wasimamizi wengi.

**MBOLEA IKIZIDI**

Kuhusu upimaji wa kiwango cha mbolea kinachohitajika kwenye bwawa kwa ajili ya ustawi wa samaki, Mwanazuoni Dk. Shoko ana ufafanuzi wa kitaalamu, akisema:

"Unaingiza mkono wako kwenye bwawa, hakikisha mkono unazama hadi usawa wa kiwiko, kisha ukunje kidogo, kama usipofanikiwa kukiona kiganja chako, ujue mbolea hiyo imezidi na ina hatari ya kuwaua samaki.

"Cha kufanya baada ya kubaini hali hiyo, ondoa hayo maji kwa kuyamwagia kwenye shamba lako, usifungulie bwawa maana maji hayo yana thamani kubwa, yana rutuba. Ukishayaondoa, weka maji mengine kwenye bwawa. Kama kiganja chako kitaonekana kirahisi, hapo ujue mbolea haitoshi kwenye bwawa."

**KUTOKA TAFIRI**

TAFIRI kupitia matokeo ya utafiti wake uliofanyika kuanzia mwaka 2004 hadi mwaka huu, inabainisha teknolojia ya ufugaji mseto wa samaki, kuku na bustani una nafasi kubwa ya kubadili maisha ya kijamii na uchumi wa mzalishaji, ikimpandisha hadhi kuelekea kwenye maisha bora akiwa kwenye mfumo mpya wa uzalishaji wenye tija maradufu.

Kwa mujibu wa ripoti ya utafiti huo uliofanywa na TAFIRI kwa udhamini wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), mfumo huo wa ufugaji mseto unamwongezea mfugaji ziada ya theluthi mbili ya alichokuwa anapata kupitia ufugaji wa kawaida; wastani wa asilimia 66 kwenye ubia wa samaki na kuku, huku bustani ya mboga ikipata ziada ya asilimia 67.

TAFIRI ambao walianza na wafugaji sita, akiwamo Mwita, sasa wanatamba na mafanikio ya darasa lao hilo, wakimtaja mfugaji huyo kuwa mfano wa kuigwa na 'kioo' kinachoakisi maendeleo ya Kanda ya Ziwa.

"Tunajivunia sana mafanikio ya Mwita, tulipomtembelea mwaka 2004, yaani ni kama alikuwa na shimo la samaki, halikuwa bwawa la samaki lile (mita tano kwa sita). Sasa anafanya vizuri Kanda ya Ziwa na kitaifa kwa ujumla.

"Kwenye maonesho ya wakulima anawavutia wengi, tumekwenda naye Kenya mara mbili, tumekwenda naye Uganda mara tatu. Kote huko wafadhili wetu amewafurahisha sana kutokana na mafanikio yake.

"Sasa kila wanapotuita kwa ajili ya mawasilisho ya mrejesho wa kazi zetu, wanasisitiza 'mje na yule mfugaji wa Tarime'. Kwa kweli ametokea kuwavutia sana kutokana na juhudi zake," Dk. Shoko anasifu.

Hali kadhalika, katika kutanua uzalishaji huo, mtaalamu huyo anasema TAFIRI wanasambaza ubunifu kwa vikundi vidogo kwenye maeneo mengine nchini, tayari wakiwa wameifikia mikoa ya Mara, Songwe, Iringa na Morogoro.

Mwanazuoni huyo wa TAFIRI, anapendekeza: "Kwa manufaa ya baadaye, elimu ya ufugaji mseto wa kuku, samaki na bustani ifikishwe kwa wakulima, wafugaji na wavuvi wadogo wengi zaidi nchini."

**WAVUVI WADOGO KITAIFA**


Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, anabainisha uvuvi wa samaki baridi unachangia asilimia 95 ya samaki wote wanaovuliwa nchini.

Vilevile, kwenye orodha ya wakuzaji samaki inayomhusu Mwita, Waziri Ndaki anataja jumla yao wako 30,064, ilhali wenzao wanaoendesha uvuvi wa moja kwa moja katika maeneo kama baharini na ziwani jumla yao wako 195,435. Kwa lugha rahisi, kundi la kina Mwita aliyeko Tarime, ni asilimia 13 ya wavuvi wote kitaifa.

Waziri anafafanua sifa ya bidhaa samaki kwamba wanachangia kupatikana asilimia 30 ya lishe ya protini yote kutoka kwa wanyama nchini; huku kiuchumi anasema sekta ya uvuvi mwaka jana (2020) ilichangia asilimia 1.71 kwenye Pato la Taifa, kiwango kinachofanana na mwaka uliotangulia (2019).

Kwa mujibu wa waziri huyo, kasi ya kukua kwa sekta ya uvuvi mwaka jana ilikuwa ya kiwango cha juu cha asilimia 6.7 kulinganisha na iliyoshuhudiwa katika mwaka uliotangulia (2019) ya wastani wa asilimia 1.5, sawa na ongezeko la asilimia 5.2 ndani ya mwaka mmoja.

Inaporejewa Dira ya Taifa ya Maendeleo (mwaka 1999-2025), mkakati uliopo wa kiserikali wa miaka mitano inayoishia 2025, ufugaji ni eneo mojawapo linalofanyiwa kazi kwa dira ya kuzalisha ajira milioni nane mahususi kwa vijana, huku ukilihakikishia taifa kujitegemea kwa vyanzo vya chakula muhimu.




Tathmini ya ukuaji wa samaki wanaofugwa kwa teknolojia ya ufugaji mseto na wanaofugwa kawaida. **Chanzo: TAFIRI Septemba 28, 2021.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kwa madai ya unyanyasaji raia, polisi wanapaswa wajitafakari

**MOJA** ya habari ambazo jana ziligonga vichwa vya habari katika magazeti mengi na uchambuzi kwenye redio na televisheni ni kauli ya Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, ya kutaka kukomeshwa mara moja vitendo vya unyanyasaji wa wananchi.

Kiongozi huyo wa ngazi ya juu katika chama tawala, alitoa kauli hiyo kwa kuwataka polisi kuacha unyanyasaji dhidi ya wananchi ikiwamo ukamataji wananchi usio na staha hususan wale wanaodaiwa kukutwa na mazao ya misitu, ikiwamo mkaa.

Shaka hakuishia hapo tu bali alilitaka Jeshi la Polisi wilayani Kahama mkoani Shinyanga kuwatazama baadhi ya askari wake wanaodaiwa kuwabambika kesi wananchi kwa madai ya kukamatwa na bangi. Hatua hiyo, bila kuuma maneno alisema hutoa mwanya kwa baadhi ya askari polisi kutumia kisingizio cha biashara ya bangi kuwakamata wananchi na kuwaweka mahabusu bila kuwafikisha katika vyombo vya sheria.

Kauli hiyo ya Shaka imetolewa ikiwa ni muda mfupi tangu Rais Samia Suluhu Hassan alipoliagiza jeshi hilo kupitia kwa mkuu wake, Inspekta Jenerali Simon Sirro, kuwa lijitafakari juu ya mwenendo wake kutokana na malalamiko ya mara kwa mara juu ya vitendo vinavyofanywa na baadhi ya askari wake.

Agosti 22, mwaka huu, wakati akifungua kikao kazi cha maofisa wa polisi, jijini Dar es Salaam, alisema Jeshi la Polisi, pamoja na mambo mengine ndilo linalolalamikiwa kuwa chanzo cha ongezeko la mahabusu katika magereza kutokana na kuchelewa kukamilisha upelelezi.

Mbali na kusababisha msongamano wa mahabusu, hivyo kuwa mzigo mkubwa kwa serikali kuhudumia watu hao, Rais pia aliweka bayana kuwa jeshi hilo ambalo limepewa dhamana ya usalama wa raia na mali zao, limepoteza imani kwa wananchi. Kwa mujibu wa Rais, hiyo ni kutokana na baadhi ya maofisa kutotenda haki kwa jamii.

Rais Samia alizungumzia hilo kwa kutoa mfano wa tuhuma za askari wa jeshi hilo kuvamia bucha kadhaa Dar es Salaam na kuchukua nyama za watu. Pia alielezea madai ya mahabusu kufia mikononi mwa polisi kutokana na vipigo, hivyo kutaka chombo hicho kuacha matumizi ya nguvu kupita kiasi.


Kwa kauli ya Shaka, ni kwamba polisi bado wanafanya kazi kwa mazoea na hata maagizo ya viongozi wa juu, akiwamo Rais, ni kama yanafika katika masikio ya viziwi kwa kuwa hayafanyiwi kazi na wahusika hawabadiliki.

Tunasema hivyo kwa sababu madai juu ya unyanyasaji wa polisi dhidi ya raia unazidi kupamba moto huku taarifa mbalimbhali katika vyombo vya habari zikifichua uovu huo. Baadhi ya askari polisi pia wamedaiwa kuendelea kuomba rushwa kwa raia na hata kutishia kuwabambikia kesi zisizo na dhamana wale wanaoshindwa kukubali masharti yao, ikiwamo kutoa fedha ili wawaachie.

Kutokana na kauli za Rais Samia na Shaka juu ya vitendo vya polisi dhidi ya raia, ni wakati mwafaka sasa kwa uongozi wa jeshi hilo kujitathmini na kuchukua hatua. Wahenga wanasema ukiona ngoma inalia sana, ujue iko karibu kupasuka, hivyo kuzidi kuwapo kwa taswira hasi kiasi cha wananchi kukosa imani nacho, ni ishara kwamba thamani yake imeporomoka.

Ni vyema viongozi waliopewa dhamana ya usimamizi wa chombo hicho, wakachukua hatua madhubuti, kwanza, kwa kuchukua hatua dhidi ya wale wanaolichafua jeshi na pili, kuwawajibisha wale waliopewa majukumu ya kulisimamia, kwa maana wa uongozi wa juu chini ya IGP.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Utii wa sheria bila shuruti ungepaswa kupewa nafasi

Na Sabato Kasika

**JESHI** la Polisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali lilianzisha kampeni ya kuiwezesha jamii kutambua umuhimu wa utii wa sheria za nchi na utaratibu wa jamii bila shuruti ili kuboresha maadili ya jamii.

Baadhi ya wadau hao ni vyombo vya dola, vyama vya siasa, taasisi za kijamii, vyombo vya habari na madhehebu ya dini, ambao wote kwa ujumla wao wana mchango wao katika kampeni hiyo.

Katika kampeni hiyo iliyoanzishwa mwaka 2012, uboreshaji huo unatazamwa kama msingi wa maendeleo yanayozingatia usalama, amani na utulivu ambavyo ni nguzo za ustawi wa kijamii, kiuchumi na kiutamaduni. Sasa ni zaidi ya miaka minne tangu kuzinduliwa kampeni hiyo ambayo ilitarajiwa kuongeza ari na moyo wa uzalendo unaozingatia uwajibikaji katika harakati za kujiletea maendeleo bila kuvuja sheria za nchi.

Hata hivyo, pamoja na kuwapo kwa kampeni hizo, bado wapo baadhi ya watu ambao wamekuwa wagumu kutii sheria bila shuruti, badala yake hadi washurutishwe hata kwa mambo yaliyopo ndani ya uwezo wao kuyatii.

Mifano iko mingi kuanzia kwa madereva wa bodaboda, ambao wanaelekezwa kubeba abiria si zaidi ya mmoja, kuvaa kofia ngumu, kusubiri taa za kuongoza vyombo vya moto ziwaruhusu wanapofika kwenye makutano ya barabara.

Lakini hayo yote baadhi yao hawayafuati hadi washurutishwe, kana kwamba hawajui kuwa sheria za usalama barabarani ambazo ni muhimu zifuatwa kwa ajili ya usalama wao na wa abiria wanaowabeba.

Badala yake baadhi yao hudaiwa kupoteza maisha au kupata ulemavu wa kudumu, kwa ajali wanazopata kwa kutotii sheria lakini bado wapo wengine ambao huenda hawataki kujifunza kutokana na makosa.

Kwenye kundi hilo la kutotii sheria, wapo wengine ambao hutupa taka ovyo hata kama wanajua ni makosa, wengine kufanya biashara kwenye maeneo yasiyoruhusiwa kisheria ikiwamo chini ya nyaya za umeme mkubwa.

Si maeneo hayo tu, bali wengine hupanga bidhaa hata pembezoni mwa barabara, hali ambayo ikitokea ajali ya gari inaweza kuwa rahisi kujeruhiwa, kutokana na kwamba maeneo waliopo si salama kwao.

Kwa mtindo huo wa kutotii sheria, wapo wengine ambao huacha kutumia madaraja yalijengwa kwa ajili yao wavuke kwenda upande wa pili wa barabara, ili kuwaepusha na ajali, lakini hawayatumii.

Badala yake wanalazimisha kuvuka barabara kwa kupishana na magari, hali ambayo inawaweka kwenye hatari zaidi iwapo hazitachukuliwa hatua za kuwashurutisha ili watumie daraja la waenda kwa miguu.

Hayo yanatokea kwenye barabara ya Morogoro, eneo la Mbezi Mwisho Dar es Salaam, ambako limejengwa daraja hilo ili watu wavuke kwenda stendi ya Magufuli au maeneo mengine, lakini wapo wasiolitumia.

Wakati hao wakifanya hivyo, wengine hujichukulia sheria mkono na kudhuru au kuua wenzao kwa tuhuma za wizi, badala ya kuwafikisha kwenye vyombo vya dola ili kuhukumiwa kulinga na makosa yao.

Mazingira hayo na mengine kadhaa, yanayoonyesha ni jinsi baadhi ya watu wameweka pembeni utii wa sheria bila shuruti na kuamua kujifanyia inavyotaka wenyewe badala ya kufuata sheria.

Ninadhani kwamba umefika wakati sasa kuongeza kasi katika utoaji wa elimu ili wale ambao hawajajua faida ya kampeni hiyo waweze kuelewa, hatimaye wasisubiri kushurutishwa.

Kwa ujumla ni kwamba, kuna faida nyingi za utii wa sheria bila shurti, ikiwamo kuiwezesha jamii kuishi salama kwa amani na utulivu na kuepusha migogoro na vurugu zisizo za lazima.

Utii wa sheria bila shururi pia unaweza kupunguza hali ya watu kuishi kwa wasiwasi wa kudhurika na matendo ya kihalifu, kupunguza watu wanaokaidi kutii sheria za nchi na kusababisha matumizi ya nguvu yasiyo ya lazima kwao.

Vilevile utii huo wa sheria unaweza kuongezeka kwa ushirikiano kati ya vyombo vya dola na jamii, kupunguza idadi ya migogoro ya kisheria inayohusu washitakiwa au walalamikaji. Hayo yakifanyika, inakuwa ni rahisi kuwa na jamii adilifu, inayojali utii wa sheria, kanuni na taratibu za nchi kwa maendeleo endelevu kuliko ilivyo sasa ambapo baadhi ya watu ni kama hawaoni umuhimu wa utii sheria bila shuruti.

# SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# *Rais Samia jicho lako liangazie uraia pacha*



Na Pascal Mayalla

**Mimi ni Mtanzania, mimi na familia yangu tulikwenda kuishi Uingereza na baadaye Marekani, mmoja wa watoto kazaliwa Uingereza, mwingine Marekani na wote ni Watanzania kwa uraia wa wazazi lakini wana haki ya kuzaliwa ya kule walikozaliwa.**

NIANZE kwa kumpongeza Rais Samia kwa kile anachoendelea kukifanya kwa ajili ya kuliponya taifa kwa kulipatia haki. Haki huliinua na kuliponya taifa na kulifanya libarikiwe.

Nimefarijika sana na tukio la kuzinduliwa kwa kituo cha haki jijini Dodoma. Huu ni uthibitisho kwamba Rais Samia si tu mpenda haki na msema haki bali ni mtenda haki, kitu ambacho ni msingi mkubwa wa falsafa haki, inayotamka kuwa: "Justice, must not only be done, but must be seen to be done." Hii ina maana kwamba haki si tu itendeke, bali pia ionekane imetendeka.

Kati ya haki kubwa kabisa duniani ukiondoa haki ya kuishi, ni haki ya uraia wa kuzaliwa. Mtu yeyote akizaliwa mahali popote, anakuwa na haki ya mahali hapo (birth right). Maisha yake yote mpaka siku anaingia kaburini, haki hii haiwezi kuondolewa.

Hii ni kama haki ya mtoto kwa mama. Baada ya mtoto kukaa tumboni kwa mama yake kwa miezi tisa, akizaliwa, aliyemzaa ndiye mama yake mpaka siku yake ya kifo. Haki hii ya mzazi iko kwa mama tu japo ili mtoto azaliwe ni lazima kuwapo mama na baba. Mtu pekee anayejua baba halisi wa mtoto ni mama.

Hivyo kiuraia, mtu akizaliwa Tanzania, nchi ya Tanzania ndiyo tumbo lake la uzazi, ndiyo maana tunaita Mama Tanzania. Mtu akizaliwa Tanzania anakuwa na haki ya kuzaliwa ya Tanzania, ni Mtanzania na haki hii kamwe haiwezi kuondolewa kwa namna yoyote hadi kifo. Hata akifa, anakuwa amekufa akiwa Mtanzania licha ya kuchukua uraia wa nchi nyingine yoyote.

Lakini kwa sheria yetu ya uraia, kutokana na kutokuwa na uraia pacha, mtu ukizaliwa Tanzania, halafu akaja kuchukua uraia wa nchi nyingine yoyote, moja kwa moja anapoteza uraia wa Tanzania wa kwenye makaratasi, yaani pasipoti, lakini huwezi kuupoteza uraia wako wa asili wa kuzaliwa Tanzania.

Mimi ni Mtanzania, mimi na familia yangu tulikwenda kuishi Uingereza na baadaye Marekani, mmoja wa watoto kazaliwa Uingereza, mwingine Marekani na wote ni Watanzania kwa uraia wa wazazi lakini wana haki ya kuzaliwa ya kule walikozaliwa.

Kwa hapa nchini, sheria yetu ya uraia inawataka wanapotimiza umri wa miaka 18, wachague moja, ama kuendelea kuwa Watanzania kwa kukana uraia wao wa kule walipozaliwa au kuukana u-Tanzania na kuwa raia wa kule walikozaliwa.

Licha ya kuwa ni mwana diasfora niliyerejea nyumbani, nilibahatika kuwa mwongozaji (event manager) wa Tamasha la Nne la Diaspora lililofanyika Zanzibar. Kilio kikubwa cha diaspora wa Tanzania ni haki ya uraia pacha. Kuna Watanzania wengi ughaibuni waliozaliwa Tanzania, lakini wakachukua uraia wa nchi wanazoishi kwa ajili tu ya manufaa ya kiuchumi au hata ukimbizi. Lakini ndani ya mioyo yao na mapenzi yao ya dhati ni Tanzania na wanajihesabu ni Watanzania kwa moyo japo kwenye makaratasi ni raia wa huko waliko.

Hoja za Tanzania kuukataa uraia pacha, pamoja na mambo mengine ni uoga wa kiusalama kama wana diaspora watakuja kujiingiza kwenye siasa za nyumbani. Huu ni uoga unaofanywa na watu wasio jiamini. Hakuna ubaya kwa Mtanzania yeyote mwenye uwezo kuwa kiongozi wa nchi yake. Tumeona kwa Barack Obama, baba yake ni Mkenya, yeye amezaliwa Marekani na amekuja kuwa Rais wa Marekani.

Kuna Watanzania wengi ughaibuni wana uwezo mkubwa kiuchumi kuja kuwekeza nyumbani Tanzania. Wamepata 'exposure' kubwa na wengine ni wataalamu wakubwa wakiwamo maprofesa ambao ni nchi za wenzetu ndizo zinafaidika na 'brain drain' yako. Wengi wako tayari kurudi nyumbani lakini wanakatishwa tamaa kupoteza u-Tanzania wao, hivyo kuamua kubaki huko huko.

Kuna Watanzania wengi waliikimbia nchi na kuwa wakimbizi kwa sababu mbalimbali. Mtu akishakuwa mkimbizi na kama hataamua kurejeshwa alikotoka ama anapewa uraia wa nchi aliyokimbilia au anapewa uraia wa nchi nyingine iliyokubali kumpokea.

Lakini ndani ya moyo wake, huyu ni raia wa nchi aliyozaliwa hadi kifo chake. Watanzania wenzetu wenye hali hii ni Watanzania, wasinyimwe haki yao ya u- Tanzania kwa kipande tu cha karatasi.

Wiki iliyopita baada ya Rais Samia kuipaisha Tanzania kimataifa kwa kuhutubia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, wiki hii kuna Mtanzania mwingine amelipaisha tena jina la Tanzania kimataifa kwa kushinda tuzo ya Nobel.

Huyu ni Abdulrazak Gurnah ambaye ameshinda tuzo ya Nobel ya Uandishi. Japo anaelezwa ni Mtanzania, kiukweli si Mtanzania. Katika makatasi yake ni raia wa Uingereza ana pasipoti ya Uingereza, hivyo kupoteza u - Tanzania wake.

Miongoni mwa watu waliompongeza Abrazaki ni Rais Samia na hii ni Tweet ya Rais Pongezi za Msemaji Mkuu wa Serikali. Pongezi kedekede zinamiminika kwa Mtanzania huyu ambaye kimakaratasi ni Mwingereza mwenye asili ya Tanzania, tena ni Mzanzibari.

Kwa vile Rais Samia umeishajitanabaisha na kujibainisha wazi wewe ni mpenda haki, msema haki na mtenda haki, tunakuomba hilo jicho lako lenye huruma, kuliangalia tena suala la uraia pacha na kuwatendea haki mamilioni ya Watanzania waliopoteza haki yao ya u-Tanzania kwa kipande tu cha karatasi.

Ili kuondoa hiyo hofu ya kiusalama iwapo tutaruhusu uraia pacha kwenye siasa zetu, tunaweza kuweka kipengele diaspora watakaoruhusiwa kushiriki siasa za ndani, ni wale tu wenye uraia pacha ambao walizaliwa Tanzania.

**pascomayalla@gmail.com**
**0754 270 403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# *Wabongo vuteni subira uhondo wa tozo waja*



Na Joseph Kulangwa

FIKIRIA, umdogo, unaumwa. Mama anakuahidi kukuletea dawa, unalalamika kuwa dawa ni chungu, anakuahidi dawa tamu ambayo utaipenda, utainywa na kupona mara moja.

Anaondoka anakweda madukani anaulizia ile dawa tamu, anaambiwa imekwisha na iliyobaki pia inatibu ugonjwa wako lakini ni chungu, inahitaji uvumilivu na ukakamavu kuimeza. Hakuna jinsi, mama anataka upone, ainunua.

Anarudi nyumbani na dawa yako anakupa. Unapionja unabaini ni chungu unaitema. Mama anakasirika kidogo lakini anakumbuka alikuahidi dawa tamu, anakukumbatia na kukubembeleza uinywe, kwa kuwa ile tamu haipatikani kwa sasa.

Unamwelewa nawe kwa shingo upande huku ukigugumia, unaibugia hivyo hivyo na kunywa maji papo hapo kupunguza uchungu, huku ukisindikizia sukari. Mama anakupa pole nawe unakwenda kulala huku ukimlaumu kimoyomoyo na kudhani anakukomoa. Utoto!

Juzi hapa nchi ya Chifu Hangaya ikakumbana na hayo. Chifu ni mfuatiliaji haswa wa mambo ya watu wake. Hakika hataki wateseke na kulalamika kuwa anawatelekeza, atatafuta kila njia awaondolee machungu yao.

Akasikia kilio cha bei ya mafuta jamii ya petroli. Kama alivyofanya kwenye chanjo ya UVIKO-19 na tozo za miamala ya simu, akaunda kamati ya kuangalia tozo za kwenye mafuta, ili ikiwezekana ziondolewe ili wese lishuke bei.

Tozo nane kati ya 23 zikabainika hazina tija hivyo zitumbuliwe. Zikatumbuliwa. Chifu Hangaya akawatangazia watu wake kuwa zimetumbuliwa, hivyo kuanzia sasa wese bei yake itashuka na maisha yatasonga kwa unafuu.

Chibulunje na timu yake wakatandika mkeka wa bei mpya ya wese siku hiyo hiyo alasiri. Kama kawaida, wasio na haraka wakasubiri magazeti kesho yake kwani walikuwa wakisubiri dawa tamu kutoka kwa Chifu Hangaya.

Asubuhi subuhi magazeti yaliyokuwa kwenye meza za wauzaji yakawa na vichwa: Nafuu bei ya petroli, dizeli; Samia abeba zigo la mafuta; Samia aagiza kushushwa kwa tozo za petroli; Bei za mafuta sasa nafuu; Rais Samia awatua zigo Watanzania; Fuel levies cut: How it will benefit public (Kuondolewa tozo za mafuta kutakavyonufaisha umma).

Vichwa hivyo vya magazeti vikaonyesha ahueni kubwa hasa kwa watumiaji wa vyombo vya moto na mitambo. Baadhi ya wasomaji wenye haraka walipokumbana na mkeka wa Chibulunje, wakaduwaa, macho kodo!

Wakakuta bei ya petroli kumbe imetoka Sh 2,427 imepanda mpaka Sh 2,439 kwa lita! Wenye ndimi zisizotulia vinywani, wakasema magazeti yamekosea kuandika bei hiyo kwa sababu ilipaswa ushuke na ndio ilikuwa msimamo wa Chifu Hangaya.

Wakajiuliza kulikuwa na sababu gani ya kuunda kamati ya kushauri kuhusu kuondolewa tozo wakati bei imepanda badala ya kushuka sasa unafuu uko wapi? Wakasahau kuwa wakati kamati inaendelea na ukokotoaji, bei ya wese huko duniani haikuwa inasubiri matokeo ya kamati, iliendelea kupanda.

Mjuaji mmoja akasema kama tozo hizo nane zisingetumbuliwa, bei ingekuwa Sh 2,600 na ushei, tushukuru kwamba zimetumbuliwa. Huyu na mwenzake mwingine, wakataka Wabongo wavute subira, kwa sababu matamu yanakuja.

Akasema hizi tozo zilizotumbuliwa ni zile ambazo hazikupitia bungeni kwamba ziliwekwa kimazingira na muktadha fulani tu ili mambo yaende lakini zile kubwakubwa ziko bungeni ndiyo sababu Chifu Hangaya anajua Bunge lina kazi ya kuzishughulikia kupitia muswada.

Kwa maana hiyo, kumbe hapana sababu ya kupiga kelele, hiyo dawa chungu tuliyomezeshwa inasaidia kuponya gonjwa hili lililokuwa linatusumbua, ina maana baada ya sheria kurekebishwa bungeni mambo yatakuwa mukide!

Ngoma sasa itabaki kwa wafanyabiashara walioagiza mafuta na kulipia tozo hizo ambazo zimetenguliwa. Itabidi sasa wakae na wahusika kina Chibulunje na wenzake waone nini cha kufanya kufidiana ili mambo yawe droo.

Lakini ili donda hili litibike, ni vyema kutafuta njia nyingine au vyanzo vingine vya mapato badala ya kuegemea kwenye wese ambalo lililemewa na tozo kwa kuamini kwamba huko ndiko watu wengi wanadakwa na hawawezi kukwepa.

Viongozi wawe wabunifu wamsaidie Chifu Hangaya kupata vyanzo vingine. Ikibidi hata kupunguzana mishahara, marupurupu na magari ya kifahari. Kwani tatizo nini? Eti waheshimiwa wabunge mwalionaje hili la mwisho?

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Siasa ziwekwe pembeni ujenzi wa hospitali ya wilaya Momba



Na Thobias Mwanakatwe

**Mpango wa kutaka kumkwamisha unatokana na msimamo wake kutetea wananchi wengi ambao wanataka hospitali hiyo ijengwe katika kijiji cha Makamba, Kata ya Chitete.**

SERIKALI ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, imemwaga mamilioni kama si mabilioni kwa ajili ya ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya katika mikoa kadhaa nchini.

Serikali imefanya hivyo ili kuwasogezea karibu wananchi huduma za afya kwa kuwa awali katika baadhi ya mikoa kwani walikuwa wakitembea umbali mrefu kufuata huduma hizo.

Kutokana na huduma za afya kupatikana kwa umbali mrefu, hali hiyo ilisababisha baadhi ya wananchi kupoteza maisha kwa kukosa huduma za matibabu hali ambayo ilizua malalamiko ya wananchi karibu kila kona ya nchi.

Ili kutekeleza azma hiyo, serikali imeamua kujenga hospitali nyingi nchini kwasababu inatambua kuwa afya maana yake ni hali ya ukamilifu kimwili, kiakili, kijamii na kutokuwepo kwa maradhi. Afya bora ni nguzo na rasilimali muhimu katika kuchangia maendeleo ya mtu binafsi, familia na nchi hususan katika kuleta maisha bora na kupunguza umaskini.

Kwa mantiki hiyo, afya inalenga kuwa na ustawi endelevu kwa jamii kwa kuzingatia mchango wa mtu binafsi kulingana na nafasi, uwezo na fursa zilizopo katika kuleta maisha bora.

Upatikanaji wa afya bora unahitaji uwezeshaji wa jamii ili kushiriki, kuamua, kupanga na kutekeleza mikakati yao ya kuwaletea maendeleo katika ngazi mbalimbali.

Miongoni mwa wilaya ambazo serikali imeamua kutatua matatizo ya huduma za matibabu ni Momba mkoani Songwe. Serikali imetoa zaidi ya Sh. milioni 900 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya wilaya.

Kinachonisukuma nizungumzie suala hili ni mvutano unaoendelea juu ya wapi ijengwe hospitali hiyo na kwa undani, mvutano umegubikwa na siasa kutaka kumkwamisha Mbunge wa Momba, Condester Sichalwe.

Mpango wa kutaka kumkwamisha unatokana na msimamo wake kutetea wananchi wengi ambao wanataka hospitali hiyo ijengwe katika kijiji cha Makamba, Kata ya Chitete.

Baadhi ya viongozi wa serikali ya wilaya, mkoa na halmashauri na madiwani wanataka ijengwe katika eneo la Tindingoma ambako wananchi wanapinga kwa sababu ni mbali na makazi yao.

Katika vikao kadhaa vya Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Momba, Sichalwe amekuwa na msimamo usioyumba wa kutaka hospitali ijengwe Kijiji cha Makamba ambacho kijiografia kiko karibu na makazi ya wananchi. Amekuwa akisisitiza kuwa hakubaliani na wazo la kutaka hospitali hiyo ijengwe eneo la Tindingoma kwa sababu itakuwa ikiwalazimu wananchi kutembea umbali mrefu kufuata huduma za matibabu kuliko ambavyo ingejengwa Makamba.

Anasema hospitali ikijengwa Makamba, itawarahisishia wananchi wote kupata huduma za matibabu kwa sababu kiko karibu na kata zote 14 za Halmashauri ya Momba tofauti na eneo la Tindingoma ambalo liko jirani na kata moja jirani na wilaya ya Mbozi.

Sichalwe anazitaka kata ambazo wananchi wake watafaidika kupata huduma kwa ukaribu iwapo hospitali itajengwa Makamba kuwa ni Nkangamo, Ndalambo, Nzoka, Myunga, Ikana, Kamsamba, Mpapa, Mkulwe, Chilulumo, Chitete na Msangano.

Katika kuweka msisitizo wa kutaka hospitali hiyo ijengwe kijiji cha Makamba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ummy Mwalimu, alimwandikia barua Agosti 18, mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Songwe akitoa maelekezo ijengwe Makamba.

Pamoja na maelekezo yaliyotolewa na waziri, kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika Agosti 27, kilipitisha ujenzi ufanyike Tindingoma badala ya Makamba kama ambavyo ilikuwa imeelekezwa na waziri.

Pamoja na msisitizo wa wizara na msimamo wa mbunge, bado Mwenyekiti wa Halmashauri, Mathew Chikoti, kwa kushirikiana na baadhi ya viongozi na madiwani wameendelea kung'ang'ania hospitali ijengwe Tindingoma.

Chikoti ambaye aliingia katika kinyang'anyiro cha ubunge mwaka 2020 lakini CCM haikupitisha jina lake, anasema maelekezo ya waziri hayakuwa ya kuamuru bali alitoa maelekezo kifanyike kikao ndicho kitoe uamuzi.

Ukiutazama mvutano huu utabaini siasa imejiingiza. Wanaotaka ijengwe katika eneo la Tindingoma wanasema hivyo kwa mtazamo wa kisiasa zaidi kutaka kumkwamisha mbunge na wao kuitumia hiyo kama turufu ya kisiasa kuelekea uchaguzi mkuu mwaka 2025.

Ziko taarifa kuwa kabla ya vikao vya Baraza la Madiwani, asilimia 70 ya madiwani walikuwa wakiunga mkono hoja ya mbunge kutaka hospitali ijengwe katika Kijiji cha Makamba lakini ghafla walibadilika baada kufuatwa na kushawishiwa na watu ambao wanajipanga kwa ubunge mwaka 2025.

Hata hivyo, asilimia kubwa ya wananchi wanamuunga mkono mbunge kutaka hospitali ijengwe Makamba ambako itakuwa katikati ya vijiji vyote vya wilaya na itakuwa rahisi kufika kwa ajili ya kupata huduma.

Niwashauri viongozi wa Momba suala la ujenzi wa hospitali wasilitazame kisiasa na kutumia mabavu kama ambavyo inafanyika sasa. Waangalie wananchi wanataka nini na pia waheshimu ushauri unaotolewa na viongozi wa juu. Katika hili tunapaswa kumuunga mkono mbunge.

Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com

**MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU MBARIKI MBUNGE WA MOMBA**

## DARASA LA NDOA

# USIRI SUMU YA USTAWI WA NDOA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

**Kama jibu ni hapana, mwenzi wako atajuaje kuwa fedha zipo au hazipo kama humshirikishi? Je, ukifa leo, mwenzi wako ana ufahamu wa fedha na mali za ndoa? Kama jibu ni hapana, huoni kuwa wewe utakuwa chanzo cha matatizo na maumivu kwa familia yako baada ya kuondoka kwako? Utamweleza nini Mungu kuhusu hali hiyo katika siku ya kiama?**

USIRI katika mambo ya fedha na mali huhatarisha uhai wa ndoa. Kukosekana kwa uwazi na uaminifu katika fedha (financial infidelity) na mali miongoni mwa wanandoa imekuwa chanzo cha migogoro mingi ya ndoa katika jamii ya leo.

Tunaishi katika nyakati ambazo tunashuhudia hali ya usiri mkubwa miongoni mwa wanandoa juu ya vipato na mali zao. Hali hii imekuwa msumari wa moto au mwiba mchungu katika mioyo ya baadhi ya wanandoa.

Imekuwa tabia na utamaduni kwa baadhi ya wanandoa kufanya vitu au mambo bila kushirikishana, kushauriana na kukubaliana.

Mfano, imetokea katika baadhi ya maeneo mke au mume anaweza kununua kiwanja, gari, kujenga au kununua nyumba, kukopa fedha benki, kusaidia ndugu fedha au kuanzisha mradi fulani bila mwenzi wake kujua. Mambo ya usiri juu ya fedha na mali yamekuwa chanzo cha migogoro katika ndoa nyingi hasa pale mke au mume anapogundua kuwa alifichwa kuhusu jambo fulani.

Usiri katika masuala ya fedha na mali huathiri uhusiano wa wanandoa. Huondoa tumaini (trust) na kusababisha hali ya kutokuaminiana; husababisha hali ya kutojiamini kwa mwanandoa (inferiority complex) hasa kwa yule aliye mwathirika wa hali hii. Pia husababisha kudumaa kwa pendo la ndoa; mwanandoa hupoteza hisia na mvuto dhidi ya mwenzi wake. Ndoa inabaki kuwa kama boksi la zawadi lililofungwa na kupambwa vizuri kwa nje, lakini ndani yake hakuna kitu.

Inawezekana kabisa kwamba wako baadhi ya wanandoa ambao hawaoni kuwa suala la uwazi ni jambo muhimu kwa sababu ya kuamini kuwa wanaishi vizuri.

Hata hivyo, ni vyema kufahamu kuwa mtu hawezi kutambua ubora wa chombo kilicho baharini mpaka dhoruba itokee.

Watu wasisubiri matatizo yatokee ndipo waone umuhimu wa kutokuwa wasiri ndani ya ndoa kuhusu fedha na mali za ndoa.

Ni muhimu na busara wanandoa wazingatie sera ya uwazi juu ya kile wanachokipata na wanachotaka kufanya. Wafikirie athari zinazoweza kutokea kutokana na uamuzi wa kuwa wasiri na waongo kuhusu vipato vyao na matumizi yao ndani ya ndoa. Mwanandoa jiulize, je, mwenzi wako anafahamu kuhusu kipato chako?

Kama jibu ni hapana, mwenzi wako atajuaje kuwa fedha zipo au hazipo kama humshirikishi? Je, ukifa leo, mwenzi wako ana ufahamu wa fedha na mali za ndoa? Kama jibu ni hapana, huoni kuwa wewe utakuwa chanzo cha matatizo na maumivu kwa familia yako baada ya kuondoka kwako? Utamweleza nini Mungu kuhusu hali hiyo katika siku ya kiama?

Wanandoa wanapaswa watengeneze mazingira ya uwazi katika maisha yao. Waepuke usiri usio wa lazima juu ya fedha na mali zao. Kama kuna hali ambayo ni kikwazo kwa mke au mume inayopelekea kutokutaka kuwa muwazi kwa mwenzake, yafaa wanandoa wajenge tabia ya kupenda mazungumzo kwa lengo la kusaidiana na kurekebisha hali iliyopo ili kuleta uponyaji katika ndoa.

Ndoa zilizofanikiwa ni zile ambazo matatizo yalipotokea, wanandoa waliyakabili kwa pamoja na umoja. Pale wanandoa wanaposhindwa kumaliza tofauti zao, wanaweza kwa nia moja kuomba msaada kutoka kwa watu wengine wenye hekima na busara na wanaowaamini kwa kuwa si afya kuishi na vinyongo.

Kuishi na vinyongo huathiri afya ya akili na mwili hata kusababisha vifo vya mapema. Kuweka vinyongo moyoni hushawishi visasi. Na kwa kweli, roho ya visasi huwa haileti suluhu bali huongeza maumivu na kuondoa uwapo wa Mungu katika maisha ya mtu. Roho ya visasi si njia nzuri ya kutatua tatizo.

Wanandoa wanapaswa kuwa na muda wa pamoja ili kupata nafasi ya kujadiliana kwa upendo na upole, kushauriana na kushirikishana hisia zao kwa kuwa mazungumzo hujenga boma zuri.

Pia Wanandoa wanapaswa kuwa na nia moja katika kuwaza, kupanga na kutenda. Uwapo wa mipango ya pamoja iliyotanguliwa na uwazi ni chanzo cha mafanikio katika ndoa na dalili njema ya watu wanaoheshimiana na kuthaminiana.

**■ Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

OKTOBA 10, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 14

## Kunywa juisi ya moto



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Tumia gharama ndogo kubadili mwonekano wa nyumba yako



## HARUSI

Ukurasa 12




## Tunza ngozi kwa asali

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | S | H | U | K | A |
| | H | | | I | |
| V | A | A | | L | |
| | M | | L | I | A |
| | B | | | M | |
| T | A | M | B | O | |

## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5




## WATOTO

# PAKA RANGI




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
INI, AMI, BWANA, JANGA, BAMIZA, NYANYA

## CHEKA



Alichokifanya Adaktari

MTOTO Prince alikwenda sokoni kununua mboga aliyotumwa nyumbani, alipofika alimkuta mchuuzi wa mbaazi akiita wateja.

**Prince:** Mbaazi unauzaje?

**Mchuuzi:** Kilo Sh.1000

**Prince:** Sema 1500, ili nirudi nyumbani nimwambie mama kuwa bei ipo juu.

**Mchuuzi:** Kwa nini? Si kakupa kiasi hicho, we nipe tu nitakupatia.

**Prince:** Nasikia mbaazi zinaumiza matumbo

**Mchuuzi:** Hapana huo ni msemo tu, hiki ni chakula kitamu sana.

**SWALI**

Zao la alizeti linapatikana mikoa mingapi Tanzania?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Vijue vyanzo vya migogoro vinavyoyatesa maisha yetu

***KARIBU tena msomaji wangu tumulike maisha yalivyo kila iitwapo leo. Wiki kadhaa zilizopita nimejadili sana kuhusu nafasi au cheo na jinsi inavyoweza kuamua hatma ya maisha yako. Ni eneo pana nitaliendeleza baadaye.***

LEO hebu tuangalie aina za migogoro na vyanzo vyake ambavyo vinasumbua sana jamii yetu. Siku zote tunahitaji kutulia na kutafakari kuhusu maisha yetu ya kila siku. Kisaikolojia watu wanajifunza vitu vingi kupitia kuona, kusikia na kusoma. Unapoongea na mtu mwingine unaweza kujifunza kwake kwa kusikia au kuona.

Hata wewe msomaji wangu yako mambo mengi unaweza kujifunza kupitia maisha ya kawaida, pengine katika malezi yako. Wako watu ambao wamewahi kufanya kitu kibaya kuhusu wewe.

Kwa hiyo unaweza kukaa na kufikiria kwamba hivi kile kilichonitokea katika maisha yangu kinaweza kurudi tena? Kuna watu wana matukio mabaya sana kwenye maisha yao ya huko nyuma.

Kwa mfano, kuna watu wamekuwa na hasira ya kufanya uamuzi ambao unachukua umauti ya watu wengine. Hili ni tatizo na changamoto. Tumeona watu wengi wamekuwa wakiamua vitu vya kushangaza.

Na kitu kingine ambacho watu wengi hawakielewi ni kwamba, hata mtu mpole huwa ana hasira na hukasirika na kuwa mtu hatari zaidi ya unavyodhania. Hata wewe kuna muda ukichokonolewa au kuchokozwa vya kutosha, hasira yako inadhihirisha huyu ni mtu hatari.

Kadhalika, ndivyo ilivyo katika maisha kwamba kuna muda inatokea mtu anahamishia hasira kwa wengine ili kupata ahueni. Baba kagombana na mama, hasira zinahamia kwa watoto.

Kadhalika, kuna muda mtu anakumbuka matukio yaliyopita na kuanza kukosa ile hamasa au mfadhaiko ambao unamfanya yeye kutengeneza migogoro binafsi. Hiyo ni hatari sana.

Tumeona watu wamewafanyia wengine vitu vya kutisha na mwisho wa siku wakahatarisha maisha yao binafsi au ya watu wengine. Hebu jiulize, je, una mgogoro binafsi ndani yako? Pengine hicho unachokishikilia sasa kina faida gani? Au umekishikilia kwa muda gani?

Na kwamba iko sababu gani na kwa nini wewe uendelee kukishikilia na umefaidika nini? Viko vitu unapaswa kuviacha na yapo mambo unapaswa kuyasuluhisha ili kufika kwenye hatma yako.

Kuna muda unapaswa uweke tamati kwa yale yanayokutesa ili mambo mazuri yaje kwako. Bila kufanya hivyo hautapata matokeo mapya. Ni vyema ukafahamu hilo na kulizingatia ili mwisho wa siku uweze kufanikiwa kwa viwango vya juu.

Lakini pia changamoto unayopitia hakikisha unaitatua. Hakuna mtu anayeweza kuishi mwenyewe kwani tunategemeana. Maisha Ndivyo Yalivyo. Ndiyo maana naandika haya maarifa ili tufaidike wote. Kama ndivyo, tatua migogoro binafsi ya kwako, lakini pia hakikisha unakuwa na amani ili mambo yaweze kusonga mbele.

Mbali na migogoro binafsi, chanzo kingine ni migogoro ya watu. Kuna muda unaweza kupitia hali ngumu sana ya maisha kwa sababu ya watu wanaokuzunguka.

Watu wanaweza kuwa ni chanzo cha kukupandisha, lakini watu hao wakawa chanzo kikuu cha kukushusha iwe ni kiuchumi na kadhalika.

Pia yakupasa kufahamu kwamba siyo kila mtu anakupenda. Si kila mmoja atafahamu thamani yako. Kuna muda inabidi uhame. Wewe siyo mti umepandwa sehemu moja ukue na kukauka hapo. Yakupasa uhame kwa kuwa wewe ni mwanadamu.

> **"Kadhalika, ndivyo ilivyo katika maisha kwamba kuna muda inatokea mtu anahamishia hasira kwa wengine ili kupata ahueni. Baba kagombana na mama, hasira zinahamia kwa watoto.**

Kwa mantiki hiyo, kuna muda unapaswa kuangalia watu ulio nao. Jiulize, je, hawa ninaohusiana nao wana faida gani kwangu? Kama wanatengeneza visasi, maneno fulani ambayo yanaweza kuchochea wewe kuanzisha migogoro na watu, wahame!

Hiyo ni kwa sababu una maamuzi ya kuhama. Usiishi kwa kufungwa na mawazo ya watu wengine kwani wewe pia una akili ndio maana Mungu kakupa ubongo ili uutumie. Kuna muda pia unahitaji kuamua vizuri na kwenda kuwasaidia watu wengine kwani hata wewe pia una faida.

Wako watu wanaoshangaza pale wanaposema: "Mimi bwana sina cha kuchangia". Una kitu pia unatakiwa ukiseme ili kiweze kuleta mabadiliko au jambo jipya.

***Msomaji, bila shaka umeelimika kuhusu aina hizo mbili za migogoro. Niishie hapa tuendelee wiki ijayo. Je, una maoni, kisa? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Ni suala la muda ila kuchanja lazima kupambana na corona

ZAIDI ya Watanzania 600,000 wamepata chanjo ya corona kutegemea aina mtu aliyojichagulia kati ya nyingi tano zinazopatikana nchini kwa sasa.

Julai, mwaka huu, Tanzania ilipokea dozi milioni moja za chanjo aina ya Johnson & Johnson chini ya mpango wa Shirika la Afya Duniani (WHO) ujulikanao kama COVAX.

Wakati chanjo hizo zikiendelea kutolewa na huku zikitarajiwa kumalizika muda wake Desemba, mwaka huu, jana Tanzania imepokea tena dozi 576,558 za Sinopharm kati ya milioni moja zinazotarajiwa kuwasili nchini.

Hadi sasa, chanjo zilizopitishwa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA) ni za Johnson & Johnson, Pfizer, Moderna, Sinovac na Sinopharm kutumika nchini kwa ambaye angependa. Chanjo hizo zinatofautiana dozi kwa kuwa ziko za mara moja na zingine mara mbili.

Jitihada mbalimbali zimefanyika kuhamasisha wananchi kukubali na kuchanja huku kukiwa na utaratibu wa makundi na kutembelea nyumba kwa nyumba na yote ikifanyika kwa hiyari.

Kuna taarifa nyingi duniani hasa kwenye mitandao ya kijamii ambazo zinahamasisha watu kutokukubali chanjo hizo kwa sababu nyingi, ikiwamo suala la utafiti lakini ufafanuzi wa wataalam unaeleza kuwa chanjo hizo ni salama.

Hadi sasa hakuna madhara makubwa yaliyoripotiwa kwa ambao wamechanja zaidi wameweza kukabili ugonjwa wa corona ambao hadi sasa hauna tiba kamili.

Kwa kawaida habari ambayo ni ya uvumi au isiyo sahihi husambaa kwa kasi na haraka zaidi,pia huaminiwa na wengi zaidi ya ile ya kweli, jambo ambalo linawafanya wengi kushindwa kufanya uamuzi sahihi kwa wakati sahihi.

Kwa sasa taarifa hasi dhidi ya chanjo zimeshika kasi hasa nchini ndiyo maana mwamko mdogo wa wananchi kuchanja unaonekana kwenye jamii na sasa kuna kazi kubwa ya kuelimisha wananchi kuondokana na imani hasi na kukubali chanjo.

Kwa mujibu wa wataalam mbalimbali duniani chanjo inaimarisha kinga ya mwili kiasi cha kwamba hata ukipata corona unakuwa kwenye nafasi nzuri ya kupona tofauti na ambaye hajachanja anakuwa kwenye hatari ya kulazwa chumba cha wagonjwa mahututi au hata kupoteza maisha.

Kwa sasa si hitaji la lazima unaposafiri kutoka nchi moja kwenda nyingine kuwa umechanjwa, bali kinachoangaliwa ni kama umepima corona ndani ya saa zilizokubalika na nchi husika na kupewa cheti kuonyesha huna maambukizi.

Kasi ya kutoa elimu ya chanjo ni muhimu hasa kwa kutumia mitandao ya kijamii na vyombo vya habari, kwamba lazima kupambana na habari hasi kwa kuwa na habari chanya za kuwezesha jamii kujua ukweli ili kufanya uamuzi sahihi.

Ni wajibu wa maofisa habari au vitengo vya habari serikalini kuongeza kasi ya kutengeneza maudhui chanya kuhusu chanjo, ili kupunguza nguvu ya ile ambayo siyo sahihi.

Katika dunia ya intaneti mwenye bando lake anajiunga na mtandao wowote na kupokea taarifa mbalimbali, inabaki kuwa wajibu wa mpokeaji wa taarifa kuchuja na kuamua kipi cha kuamini na kipi cha kuacha.

Je, ni kwa kiasi gani jamii yetu hasa maeneo ya vijijini wanaweza kutofautisha habari za uongo na kweli ili kufanya uamuzi sahihi ndipo umuhimu wa kutengeneza maudhui sahihi kwa wingi kwa ajili ya kulisha jamii?

Hakuna ubishi kuwa chanjo ya corona ni muhimu sana na huenda ikafika wakati bila chanjo huwezi kupata huduma fulani, kwa kuwa upo ushahidi ambao nchi zilizofanikiwa kuchanja watu wake kwa asilimia 100 sasa hawana maabukizi wala vifo vya ugonjwa huo.

Elimu sahihi kwenye mitandao ya kijamii na vyombo vya habari pamoja na ubunifu katika kuwafikia wananchi kutaongeza idadi ya wanaokubali kuchanja na huenda dozi zote zikaisha na kuhitajika nyingine.

Hadi sasa katika nchi yenye zaidi ya Watanzania milioni 60 waliochanja hawafiki mil moja, maana yake lazima ifanyike kazi ya ziada kuwaelimisha wananchi umuhimu wa chanjo na hasa watumishi na viongozi wa umma kuonyesha kwa vitendo.

***Mungu ibariki Tanzania***

# HARUSI











Ukitaka kuifanya harusi yako ionekane ya Kiafrika zaidi ni jambo linalowezekana. Kuanzia chakula, mapambo hadi mavazi unaweza kuyaweka katika uasilia, pichani ni baadhi ya mavazi ya harusi yaliyotengenezwa kutokana na mitindo ya Kiafrika.

# MITINDO







## 'SHINGO NDEFU' Fulana zinazowadatisha 'masharobaro'

VAZI la fulana za shingo ndefu umekuwa maarufu miongoni mwa vijana, kutokana na mwonekano wake kuwa wa kupendeza zaidi.

Nguo hizi ambazo zinavaliwa katika kipindi cha baridi, hivi sasa limekuwa vazi la wakati wote kutokana na kupendwa na idadi kubwa ya watu.

Baadhi ya wabunifu wameongeza vionjo na nakshi na kulifanya kuwa chaguo la kipekee kwa watu maarufu kama wanamuziki, wasanii wa filamu na vijana wa kawaida.

### CHAGUA KWA USAHIHI

Endapo unapenda kuvaa nguo ya aina hii, unatakiwa kuhakikisha mtindo na rangi ya nguo unaendana na wewe.

Hakikisha ubora wa kitambaa, kabla hujaangalia vionjo vingine.

Chagua rangi nzuri na ukubwa unaolingana na mwili wako, kwa sababu ukikosea unaweza kuondoa uhalisia wa mwonekano wako.

Angalia shingo kama inavutika kwa sababu inatakiwa kutanuka na kurudi katika ukubwa wake wa awali. Endapo ukiona inatanuka bila kurudi, basi hiyo sio halisi.

Fulana ya aina hii, unaweza kuvaa na Jeans, suruali ya kitambaa au ukatumia kama nguo ya ndani ya suti.



UREMBO

# Tunza ngozi kwa asali

NGOZI isiyo na kasoro kwa mwanamke humwongezea ujasiri na kujiamini.

Kuna njia nyingi za utunzaji wa ngozi ikiwamo kutumia vipodozi vya viwandani na vyakula asili'.

Katika kukupa urahisi wa kuweka ngozi yako salama zaidi huku uking'aa, nitaeleza namna unaweza kutumia asali kuongeza umaridadi.

**KULAINISHA NGOZI**

Asali hutumika kulainisha ngozi na ina asili ya kuvuta unyevu kutoka kwenye hewa na kuipa ngozi uwezo wa kuhifadhi unyevunyevu, hivyo ni faida kwa mtu mwenye ngozi kavu.

Chukua asali mbichi kijiko kimoja cha chai kisha paka usoni, kaa nayo kwa dakika 15 hadi 20 kisha safisha uso wako.

**KUSAFISHA NGOZI**

Asali ina uwezo wa kusafisha ngozi, kutibu na kuzuia chunusi.

Pia asali inaua bakteria na kuvuta uchafu katika matundu ya ngozi, matumizi yake yatakusaidia kutatua tatizo la kuota kwa chunusi.


Chukua asali mbichi kijiko kimoja cha chakula, changanya na mafuta ya nazi vijiko viwili kisha paka usoni huku ukisugua taratibu kwa kufanya kama viduara na epuka kufikisha machoni. Ukimaliza kusugua uso, osha uso wako kwa maji ya uvuguvugu.

**KUSUGUA NGOZI**

Changanya kijiko kimoja cha asali na kijiko kimoja cha baking soda.

Tumia mchanganyiko huu kusugua ngozi yako. Asali inaongeza lishe na chembe chembe kuzuia madhara yanayotokana na sumu za hewani zinazozeesha ngozi. Baking soda inasaidia kusafisha matundu ya ngozi.

Asali inasaidia kuboresha ngozi iliyoungua na jua na kurudi katika mng'ao wake wa asili.





MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Muandae mtoto wa miezi sita kula



LISHE ni msingi bora wa kumlea mtoto mwenye afya bora.

Kwa mtoto anayeanza kula, ni muhimu apewe chakula kiasi kidogo ili kumfanya azoee. Si mara zote watoto hupenda vyakula mara ya kwanza, lakini baada ya muda huzoea na kukipenda.

Mtoto wa kuanzia miezi sita anayeanza kula apewe chakula laini kwa kipimo cha kijiko kimoja, mara tatu kwa siku.

Kwa kila baada ya siku tatu hadi wiki endelea kuongeza idadi ya vijiko, wingi, uzito na aina ya chakula.

Ni muhimu kutochanganya vitu vingi wakati mmoja, maana mtoto anaweza kupata allergy kutokana na vyakula na ukashindwa kuelewa nini kimesababisha.

Jinsi mtoto anavyozidi kukua boresha chakula chake taratibu kwa kutumia mafuta yenye afya, hasa yale yatokanayo na mimea na viumbe wa baharini akiwamo samaki.

Kutokana na ushauri wa wataalamu wa lishe, mtoto mwenye miezi 6 huanza rasmi kupewa vyakula vya ziada huku akiendelea kupewa maziwa ya mama.

Ni vizuri kuzingatia kuwa, mtoto anayeanza kula vyakula asichanganyiwe vyakula tofauti muda wa mwanzo. Anza kumpa kitu kimoja ili kufahamu anapendelea vyakula gani zaidi na vipi hapendi.

Mpe zaidi vyakula anavyopenda, huku ukiwa unamchanganyia vyakula asivyopendelea kwa kiasi kidogo. Hii itamfanya azoee vile vyakula asivyopenda na kuanza kuvipenda pia.

Hii husaidia pia kufahamu vyakula ambavyo vinaweza kumletea mtoto madhara.

Aina ya vyakula anavyoweza kula mtoto wa umri huo ni uji laini, viazi lishe, mboga za majani zilizopikwa na kuiva vizuri na matunda yalivyopikwa, kuiva vizuri na kupondwa. Mfano wa vyakula na matunda ni boga, tufaa, ndizi na peasi.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



## Dondoo za kuchagua mito ya mapambo



UNAWEZA kubadilisha mwonekano wa ndani kwa kuongeza haiba ya kipekee kwa kutumia mito ya viti. Hata hivyo una hitaji umakini wakati unapofikiria aina hii ya mapambo, hizi ni baadhi ya ndondoo muhimu kuzifuata wakati wa kununua mito ya mapambo.

**1:** Chagua mitindo mizuri ya mito ambayo itaendana na sofa zako. Unaweza kuchagua aina ya mitindo kulingana na mazingira, tabia na mapenzi ya mtu husika.

**2:** Kama unataka kuweka tofauti na sofa, hakikisha unachagua mito yenye maumbo ya kufurahisha kama mviringo, pembe tatu, moyo au wanyama.

**3:** Chagua rangi nzuri na yenye kuvutia pale unapoweka ndani au sehemu yoyote. Mito inapendeza zaidi kama ikiwa na rangi tofauti katika sehemu moja.

**4:** Angalia ubora wa vitambaa na foronya ili kukuhakikishia kudumu kwa muda mrefu zaidi.

# Tumia gharama ndogo kubadili mwonekano wa nyumba yako

BAADA ya miaka kadhaa ya kuishi kwenye nyumba, wengi hutamani kubadilisha mwonekano.

Mara nyingi wamiliki wengi wa nyumba hupendelea kurekebisha jengo au kununua samani mpya ambazo hutumia gharama kubwa. Lengo la makala ya leo ni kukupa mwanga tu namna ya kuboresha maisha ya nyumbani kwako kwa gharama nafuu na ukabaki unafurahia maisha.

Kumbuka kwamba si tu matumizi makubwa pekee ya pesa ambayo yanaweza kubadilisha au kuleta mavuto wa nyumba bali hata kwa gharama kidogo tu ya pesa hiyo ina uwezo wa kuipendezesha.



Kwa mfano, matumizi tofauti ya rangi, karatasi za ukutani, vitambaa na malighafi zingine zilizotengenezea samani zako vina nafasi kubwa ya kubadilisha kabisa mwonekano wa nyumba yako na kukupa wa kuvutia zaidi.

Mathalan, kupaka rangi upya kabati la luninga, miguu ya kiti au meza, kubadili kitambaa kilichotengenezea viti au sofa, nako kunasaidia kubadilisha mwonekano katika nyumba yako.

Nyingine ni kubadili vitu kidogo kama vile tai na fimbo za pazia, mapazia yenyewe, zulia, mapambo ya ukutani na mengineyo.

Viko vitu vingi ambavyo unaweza kuvifanyia marekebisho kwa gharama ndogo ndani ya nyumba yako na ukaifurahia tena na usiichoke. Kwa mfano kubadili rangi ya ukuta nayo ni mbinu nyingine.


Pia hata kuchagua kubadili kitu kingine unachoona unatakiwa kufanya hivyo, kama ni foronya unatakiwa kuangalia zile zinazoendana na zilizoko kwa wakati wa sasa.

Kama vitu vyako vya ndani umevitumia kwa miaka mingi na vimepitwa na wakati ndiyo maana huenda vinakuchosha na kuiona nyumba yako mbaya, usiikatie tamaa kwa sababu inawezekana kuirudisha katika ubora wake.

Kikubwa ni kuwa mbunifu na kuongeza kidogo kidogo vionjo vinavyoendana na wakati katika nyumba yako hiyo. Hata kama huna kipato kikubwa inawezekana na kwamba si lazima uweke vyote kwa pamoja, lakini kadri unavyojaaliwa unabadili cha zamani na unaweka kinachoendana na wakati wa sasa.Utanunua pazia leo lakini siku nyingine kitu kingine na hii pia itasaidia nyumba yako kuonekana mpya kila siku.

Ni ukweli kuwa vitu vya nyumbani vinabadilika kila baada ya kipindi Fulani. zulia ulilonunua miaka mitano iliyopita, haliwezi kuendana na wakati wa sasa.

# KATUNI


JUKWAANI
KATUNIKA KI'DOMOKRASIA!
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
MILO MITATU
KHA!
MKEO ANGEKUWA ANAKUPENDA ANGE-KUACHA UJE KWANGU?
KWA TAARIFA YAKO HUKU KWAKO NAFANYA "FILDI TU"
NIMEMUAHIDI MWENYE NYUMBA APITIE AONE KAZI INAVYOYUMBA!
MKEO AMEANDIKA TALAKA!
MLENGWA NANI KABLA SIJAUA!
UKIELIMISHWA UNATOA 'BEGA' MWENYEWE! BILA MBINDE
KUNA MBISHI KAMA MIYE!.. "TAYARI"
WEEE!
AFYA SIO SIASA
MIE SINDANO YOYOTE! NIKIIONA TU! NAZIRAI
NENDA KWA MKEO
SIJAWAHI KUONA POPOTE KITANDA KUWA KATIKATI "HAPA SI BURE!"
'UKICHANJA' UNAJIAMINI HATA BIERE INASHUKA...
"NIMECHANJA MBUGA" KUSAKA WATEJA LAKINI 'BILA BILA'
HA HA HAAA!!! ACHA UBOYA NILIDHANI UME-CHANJA YENYEWE!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...UKIONA KAPENDEZA, MWENZAKO KAWEKEZA

## HABARI KIMATAIFA

# China yasisitiza lazima muungano na Taiwan

**BEIJING,** CHINA

RAIS wa China Xi Jinping, amepigilia msumari katika mvutano unaoendelea na kisiwa cha Taiwan, akisema muungano wa pande hizo lazima utimizwe.

Kiongozi huyo alisema muungano unastahili kufikiwa kwa njia ya amani, lakini alionya kwamba watu wa China wana utamaduni unaopinga utengano.

Hata hivyo, Taiwan ilijibu tamko hilo kwa kueleza hatma yake iko mikononi mwa watu wake.

Taiwan inajichukulia kama taifa huru, huku China ikiitaja kama mkoa wake uliojitenga.

Serikali ya China imefuta uwezekano wa kutumia nguvu kufikia muungano huo

Rais Xi ameingilia suala hilo baada ya China kutuma idadi kubwa ya ndege za kijeshi katika eneo la ulinzi wa anga la Taiwan katika siku za hivi karibuni.

Baadhi ya wachambuzi wanasema hatua hiyo huenda ni onyo kwa Rais wa Taiwan wakati kisiwa hicho kinaadhimisha sikukuu ya kitaifa leo. Waziri wa ulinzi wa Taiwan, alisema mvutano wao na China umekuwa mbaya zaidi katika miaka 40 iliyopita.

Hata hivyo, matamshi ya Rais Xi yalionekana kuwa ya maridhiano zaidi na Taiwan ikilinganishwa na tamko la Julai, ambapo aliahidi kuvunja jaribio lolote la uhuru wa kisiwa hicho.

Akiongea katika hafla ya kuadhimisha miaka 110 ya mapinduzi ambayo yaliangusha nasaba ya mwisho ya ufalme wa China. mnamo 1911, alisema umoja kupitia njia ya amani ni bora zaidi kwa masilahi ya taifa la China na wenzao wa Taiwan.

"Hakuna mtu anayepaswa kudharau uamuzi thabiti wa watu wa China, dhamira thabiti na uwezo mkubwa wa kutetea himaya yake." Alisema rais Xi Alisisitiza "Jukumu la kihistoria la kuungana tena nchi yetu lazima litimizwe, na hakika litatimizwa,"

Rais huyo alisema anataka kuona muungano ukifanyika chini ya nchi moja, mifumo miwili kama ilivykuwa kwa Hong Kong, ambayo ni sehemu ya China lakini ina kiwango cha juu cha uhuru.

Ikulu ya Taiwan ilisema kwamba maoni ya umma yalikuwa wazi dhidi ya sera ya nchi moja, mifumo miwili.

**BBC**



Mfanyakazi wa uokoaji akitazama jingo lilotumika makazi ya watu iliwa limeporomoka bila kusababisha maafa kwa watu katika mji wa Bangalore nchini India juzi **(PICHA: AFP)**

# Ethiopia yawashambulia waasi waliovamia Amhara

**ADIS ABABA,** ETHIOPIA

WANAJESHI wa Ethiopia na washirika wake wanaendelea kufanya mashambulizi ya anga na ardhini dhidi ya waasi wa Tigray. Mapigano yaliyoambatana na ulipuaji mabomu yalishuhudiwa Alhamisi na Ijumaa dhidi ya waasi hao wa kundi la TPLF Kaskazini mwa Mkoa wa Amhara.

Ripoti hiyo ni kwa mujibu wa vyanzo kutoka kwa waasi na wahisani. Mashambulizi hayo yamefanywa huku kukiwa na minong'ono kuwa kuna ari kubwa ya vikosi vya serikali kuwakabili waasi.

Ripoti hizo zilitolewa siku chache baada ya waziri mkuu Abiy Ahmed, kuapishwa katika muhula mpya wiki iliyopita ambapo aliapa kuilinda heshima ya Ethiopia.

Hata hivyo kuna ukosoaji wa kimataifa kuhusu mgogoro huo.

Vita katika eneo la Tigray, ilianza mwezi Novemba baada ya waziri mkuu Abiy, kutuma wanajeshi kukiondoa chama cha TPLF ambacho ni chama tawala cha eneo hilo na watawala wa zamani wa taifa hilo.

Hatua ilichukuliwa kwa kile alichosema ilitokana na mashambulizi ya TPLF katika kambi za jeshi za taifa hilo.

**DW**

## Mmoja afariki kwa Ebola DRC

**KIVU KASKAZINI,** DRC

MTU mmoja ameripotiwa kuambukizwa kirusi hatari cha Ebola katika Mkoa wa Kivu Kaskazini nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Kulingana na taarifa za Shirika la Afya Duniani (WHO) iliyotolewa juzi, aliyeambukizwa ugonjwa huo ni mtoto mdogo ambaye aliyefariki duniani siku ya Jumatano baada ya muda mfupi kuonyesha dalili za kuwa na Ebola.

Hayo ni maambukizi ya kwanza kuripotiwa tangu ilipotangazwa rasmi mwezi Mei mkoa wa Kivu Kaskazini kuwa ugonjwa huo umemalizika.

Mkurugenzi wa WHO kwa Afrika, Matshidiso Moeti alisema shirika hilo linasaidiana na serikali ya Kongo kufanya uchunguzi.

Mtoto huyo alikuwa akiishi karibu na mji wa Beni, kitovu cha kibiashara na kinachopakana na nchi jirani za Rwanda na Uganda.

Mji wa Beni umewahi kukumbwa na maambukizi ya Ebola kwa muda mrefu kati ya mwaka 2018 na 2020, kulingana na rekodi za WHO.

## Trump azuia uchunguzi uvamizi wa Capitol Hill

RAIS wa zamani wa Marekani Donald Trump, inaelezwa anajaribu kuzuia uchunguzi wa kamati ya bunge ambao unataka kubainisha chanzo cha uvamizi wa jengo la Bunge Capitol Hill uliofanywa mwanzoni mwa mwaka huu. Magazeti ya Washington Post na Politico yanadai kwamba wamepokea barua kutoka kwa wakili inayosema kwamba washirika wa zamani wa Trump wanaombwa wasitoe ushahidi mbele ya kamati hiyo. Wafuasi wa Trump walilivamia jengo la Capitol Hill mnamo Januari 6, mwaka huu na kusababisha watu watano kuuawa.

Trump alishutumiwa kwa kuwachochea washambuliaji hao.

Rais Joe Biden, juzi alikataa ombi la mtangulizi wake kuzuia nyaraka zinazohusu shambulio hilo kuwasilishwa kwa kamati hiyo ya bunge inayofanya uchunguzi.

Trump alitaka afanyiwe upendeleo na kupewa kinga kama kiongozi wa zamani wa nchi hiyo.

**DW**

SAFU

## MAKALA

# KUTOJIAMINI NI SAWA NA MTU KUWA GEREZANI



Na Magabilo Masambu

GEREZANI ni mahali ambako watu wanalazimishwa kukaa wakishikiliwa kinyume cha matakwa yao, ama wakiwa wamehukumiwa au wakiwa wanasubiri hukumu zao. Kwa kawaida hali ya kufungwa ndani ya gereza ni adhabu itolewayo na mahakama kwa mtu aliyevunja sheria baada ya ushahidi usiotia shaka kutolewa.

Tutakubaliana kwamba si watu wote wanaofungwa magerezani wanakuwa na hatia, wakati mwingine kwa uonevu tu. Baadhi ya nchi huko duniani zimekuwa zikitumia magereza kufunga watu ama wanaowapinga viongozi au wanaokosoa serikali zao ikiwa njia mojawapo ya kuwanyamazisha.

Hali hii ndiyo inayowakuta watu wengi kwenye maisha. Unaweza kudhani kwamba uko huru lakini ukawa uko gerezani bila kujitambua. Tunatembea tukiwa magerezani kama ambavyo mfungwa hana uhuru wa kufanya jambo lolote isipokuwa awe amepewa amri. Ndivyo ilivyo kwetu sisi tunaodhani tuko huru tunashindwa kufanya mambo yetu vilevile.

Kutojiamini kunajenga woga na woga huleta hofu mwisho wa siku hakuna kitakachoweza kufanyika kwa kuamini kwamba huwezi kufanya hiki na kile na kwamba unahitaji fulani kukusaidia kufanikisha jambo lako.

Sikatai kwamba ili kufanikisha mambo yetu, tunawahitaji watu nafahamu kuna kutegemeana lakini tunapowahitaji lazima tuwe tunaweza kujibeba. Kupenda kubebwa kumekuwa kwingi kiasi cha kutufanya tushindwe kujisimamia katika yale ambayo tunayajua na ambayo ndiyo yangeweza kutusaidia zaidi.

Kutojiamini ni ugonjwa unaofifisha uwezo wa kufikiri na badala yake hupumbaza na kukufanya ujipendekeze ili upate unachokusudia na zaidi kuyaona mambo kinyume kitu ambacho mara nyingi huwafanya watu wanaojua uwezo wako katika eneo fulani, kushangazwa kama wewe ndiwe.

Kuna watu wana elimu za vyuo vikuu lakini wameshindwa kuzitumia au kutumia uwezo wao mwingine wa vipawa walivyo navyo kutatua matatizo yao kwa kudhani kwamba kila wanachofikiri kufanya hakitakuwa sahihi kwao. Badala yake huona ili kuzikwepa changamoto hizo ni kuongeza elimu zaidi wakidhani kwamba wataziepuka kitu ambacho si kweli.

Kuna watu wanaamini kwamba mustakabali wa maisha yao uko mikononi mwa watu wengine na kwamba bila hao maisha yao hayapo. Lakini ni vizuri kufikiri kwamba kama miongoni mwao hakuna aliyeamua uzaliwe basi hakuna atakayeamua uwe nani?

Wangapi katika maisha tumewahi kufikiri kuwa mtu fulani na hatujawa? Leo hii kila mtu ukimuuliza atakwambia nilitamani sana niwe fulani. Wako waliotamani kuwa mahakimu, walimu, polisi, wanajeshi, marubani lakini hawajawa. Tafsiri yake ni kwamba anayepanga uwe nani ni Mwenyezi Mungu, hivyo lazima uitazame nafasi uliyo nayo kama nafasi unayostahili japo bado unaweza kuendelea kufanya juhudi ufike ulikopangiwa kufika.

Wasiojiamini wengi huwategemea sana wanadamu katika kutimiza malengo yao na pale wanadamu hao wanapotoweka watu hawa hubaki katika wakati mgumu sana, hata maandiko yanasema: "Amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu kuwa kinga yake na moyoni mwake amemwacha BWANA, maana atakuwa kama fukara nyikani palipo ukame katika nchi ya chumvi isiyokaliwa na watu." (Yeremia 17:5-6)

Sifa kubwa ya watu wasiojiamini wanakula na kuywa kwa kusifu watu waliofanikiwa ama wanaodhani wanaweza kuwasaidia kupata au kuwa mahali fulani. Hapa kwetu kwenye eneo la siasa na uongozi, hili limeonekana zaidi katika kutafuta madaraka.

Lazima ufike wakati tutakaoweza kuamini kwamba tunaweza kuendesha maisha yetu bila madaraka ya kisiasa labda iwe imeandikwa na kama ndivyo, bado hakuna atakayeweza kukwamisha hilo bali akipatikana atakuwa na nafasi ya kuchelewesha tu.

Hatari yake ni kwamba wale wanaosifiwa wakijiingiza kwenye mtego huu wa kuamini kwamba sifa hizo wanazistahili, maana yake taifa litapata viongozi wasiokuwa na uwezo au wenye uwezo watakaokuwa tayari kutoutumia uwezo wao kwa hofu ya kupoteza nafasi za madaraka, hivyo nyekundu kusemwa kuwa ni nyeupe huku wakiona ni nyekundu.

"BWANA wa majeshi ameapa akisema hakika yangu kama vile nilivyoazimia ndivyo itakavyokuwa na kama nilivyokusudia ndivyo itakavyotokea." (Isaya 14:24). Ibrahim na Sara katika uzee wao wakapata mtoto kwasababu ahadi ya Mungu ilikuwa palepale pamoja na kwamba Ibrahimu alijaribiwa akazaa na kijakazi bado jaribio hilo halikuzuia ahadi ya Mungu kwao.

Tunao mfano halisi leo kwamba Nelson Mandela alifungwa miaka 27 gerezani lakini bado kusudi la Mungu la yeye kuwa Rais wa kwanza mweusi Afrika Kusini likawa palepale. Hofu ya nini? Nani aliyewahi kufikiri kwamba ipo siku Tanzania itapata Rais mwanamke? Lakini leo tunaye na mambo mengine yatakuwa hivyo.

Kwa hiyo kuna mambo mengi ya ujifunza na kuondoa hali ya kutojiamini badala yake tufanye yale tunayoona yako sahihi kwa wakati sahihi bila kutegemea watu wengine watufanikishie ndoto zetu. Ukijiamini utakuwa na uwezo wa kujaribu kufanya mengi na katika hayo mengi utajikuta njia zako za mafanikio zimo humo humo.

Wengi tunashindwa kufanikiwa kwa kutojaribu wenyewe kwasababu hatujiamini na hivyo tumo gerezani ingali tunatembea.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Chura, Kuku na Yai, taarabu zilizotikisa*



Na Adam Fungamwango

**'Mdudu Ndani ya Kokwa la Embe Kaingiaje', halafu wakarudi tena na wimbo wa 'Kuku na Yai' kinachouliza kuku na yai nini kilianza. Huu uliimbwa na Elizabeth Sijila.**

CHURA nakuulizia unipe jibu makini kwa kila ijapo mvua wakimbilia bwawani. Huna nguo ya kufua na wala hauna sabuni, nijibu yapate tua, maji utayafanyani. Chura punguza vituko na wako uhayawani, umezua sokomoko watu hawaelewani. Ukivunjika mgongo, dawa atakupa nani?"

Ni baadhi ya maneno maarufu yaliyomo kwenye kibao cha taarabu kilichotikisa mwanzoni hadi mwishoni mwa miaka ya 1980. Yeyote yule aliyekuwa mtoto, kijana au mkubwa kwenye miaka hiyo atakuwa anaujua wimbo huu.

Mara kwa mara ulikuwa ukipigwa na kuombwa na wasikilizaji wengi kwenye Redio ya Taifa kwa sasa, wakati huo ikiitwa Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD). Ni moja ya nyimbo bora kabisa za muziki wa taarabu asilia enzi hizo zilizowahi kutokea.

Ulipigwa na kundi la JKT Taarabu, ukiimbwa na Patricia Hillary. Kundi la JKT Taarab lilikuwa moja ya makundi bora kabisa wakati huo ya muziki. Pamoja na kumiliki wanamuziki wenye vipaji vya hali ya juu, lilitoa nyimbo nyingi zilizotikisa na kupendwa mno miaka ya 1980.

Kwenye miaka ya 1970, mbali na nyimbo nyingi tamu za taarabu, wimbo uliokuwa bora kabisa wakati huo ulikuwa ni 'Sabarkheri Mpenzi', ambao ulivuma kama moto nyikani.

Ni wimbo ambao hadi wasanii wa kizazi cha sasa, wamekuwa wakiurudia kwa mitindo mbalimbali. Hata wasanii Aslay na Nandy juzi juzi tu waliurudia. Ukweli tu ni kwamba, wimbo huo ambao asili yake ni Zanzibar, ulirudiwa na wanamuziki wengi sana.

Ikaja miaka ya 1980 ambapo kulikuja na mapinduzi makubwa ya muziki wa taarabu, hasa Tanzania Bara. Kuliundwa makundi mengi na wanamuziki, wengi walikuwa wanachukuliwa kutoka Zanzibar na Tanga ambako kiasili inasemekana ndiko kwenye wasanii wazuri zaidi wa muziki huo ingawa hata mikoa mingine baadaye walitokea wengi wakawa mahiri sana.

Wanamuziki wa Taarabu wa Tanzania, wakavuka nchi hadi Burundi ambako walikwenda kuunda makundi mawili hasimu, Shaan Musical Club na Jasimine Musical Club, ambayo nayo hayakushikika kwa kutoa nyimbo zilizotokea kuwa bora, si Burundi tu, bali Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Muongo mzima wa 1980, makundi yalishusha nyimbo kwa kushindana. JKT Taarab wakatoa wimbo wa 'Mdudu Ndani ya Kokwa la Embe Kaingiaje', halafu wakarudi tena na wimbo wa 'Kuku na Yai' kinachouliza kuku na yai nini kilianza. Huu uliimbwa na Elizabeth Sijila.

Egyption Music Taarab kutoka Zanzibar wakadondoka na wimbo hao 'Pendo Linaua', ukiimbwa na Afua Suleiman, Bima Taarab nao hawakukubali, wakalipa na wimbo wa 'Tunapendana kwa Dhati'.

'Ni bure zenu fitina, sisi wala hatuzijali. Wenyewe tumependana, kuachana ni muhali.' Yalikuwa ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye kibao hicho, kilichoimbwa na marehemu 'Mariam Naylon.'

JKT Taarab kama kawaida yao, wakashuka na wimbo 'Ukewenza'. 'Somo aliyenifunza mafunzo nazingatia, Siogopi ukewenza mume akishaamua, katu sijajikimbiza, mwenzangu kumkimbia, nitamtunza mume wangu kama ilivyo sheria, nizidishe penzi langu, mapeshi kunisifia, nije mpiku mwenzangu na mbwembwe kumtilia.

Mume akishaamua kuweka ukewenza, katu usije kimbia, mwenzako atajikweza.' Maneno haya yamo kwenye wimbo huo.

Patricia, alirudi tena na wimbo 'Njiwa Peleka Salamu' namba moja ambao ulikuwa maarufu, halafu baadaye akatoa namba mbili yenye maneno yafuatayo:-

"Njiwa usimlaumu kosa ni wako muhibu, njiwa kampa salamu yeye akamgilibu."

JKT Taarab hawakupoa, wakaja na wimbo 'Jamani Mapenzi Yananitatiza' mwimbaji Patricia, lakini pia wakampa Sijila wimbo wa 'Nahodha kukaa Nyuma.'

Dhamira Musical Club, wakaja na wimbo wa 'Kifo cha Mama' na 'Kilio cha Baba'. Kikundi kidogo cha Makutano Dancin Troupe cha Manzese Uzuri, kilikuwa na taarabu yao, kikarekodi wimbo uliokuwa maarufu 'Siku yako ipo Nimekuwekea.'

'Siku yako ipo mwanangu nimewekea, ukishageuka upepo usije kulia, kuna siku iso jina, zamu yako itafika, usidhani nyongo sina ewe swahiba pulika, utendayo nayaona lakini nayalimbika, siku yako iko mwanagutu nimekuwekea utapogeuka upepo usije kulia. Siku hiyo utanuna kama hujapatacheka , na mafunda kukutuna lau kama utapasuka, mito utaitafuna uzirarue na shuka.' Ni wimbo uliotikisa mno.

Shaan wao walitoa wimbo maarufu wa 'Sina Zaidi ya Wewe', Jasmine wao wakajibu wa wimbo wa 'Pendo kazi Yetu.'

# HADITHI

MAPENZI ni nini? Si kumpenda yule unayemtaka wewe? Kwa nini inafika wakati watu wanapangiana? Je, ukilazimisha yanaitwa mapenzi? Si yatafanana na utumwa? Yeyote anayetaka kulifanya penzi liwe na matabaka, rangi, kabila, anaweza kusababisha maafa makubwa. Donald, kijana msomi aliyetoka Marekani, anarejea nchini Tanzania. Akakabidhiwa kuendesha kampuni za baba yake lakini pia anatakiwa aoe. Hapo ndipo tatizo linapoanza. Endelea na uhondo huu wa kusisimua.

# Sumu ya Mapenzi-27

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Sikiliza wewe." Sasa ilikuwa sauti ya Chiko. Nitakutandika bastola ya kichwa. Utakufa, halafu tutakwenda kukutupa baharini uwe chakula cha samaki. Sidhani kama polisi au mtu yoyote atajua nini kimetokea. Mimi ndiye pia nitawaua wazazi wako. Nitajua watakufa kwenye mazingira gani, lakini lazime wawe marehemu." Aliongea kwa kujiamini.

"Simu yangu mliipata?" aliuliza.
"Tukuulize wewe?"
"Sikuona."
"Na ndicho tulichokuwa tunakitaka. Nilituma vijana waitafute na walikusachi sana ulipokuwa umepata ajali hawakuiona. Tukajua tu itakuwa imesagikasagika. Ila walikuwa waoga, walidhani umeshakufa, wangekuulia pale pale." Chiko alijigamba.

"Doroth nakuomba, niueni mimi, lakini msiniulie wazazi wangu." Vicheko kutoka kwa wapenzi wawili Doroth na Chiko vilitawala.

"Utakuwa umeshakufa. Huna haki ya kutaka kujua tena duniani kuna nini. Ukishakufa, huku duniani tuachie wenyewe tujue nini tutafanya," Chiko aliongea kwa kejeli.

"Enhe, niambie mpenzi wangu, kabla ya kumuua huyu kwanza, tumfanye nini? Tumtese. Au tuwe tunamkata kiungo kimoja baada ya kingine?" Chiko alimuuliza Doroth.


"Ya nini yote hayo? Afe tu leo hii hii ili kesho tuanze harakati zetu za kuoana. Yeye si alikuwa hanitaki?"

"Chiko alikenua meno. Akatoa tabasamu ambalo si halisi "Tena ndugu yangu utakufa kifo cha ajabu sana. Hakuna atakayejua kama umekufa. Hata polisi wenyewe watakusaka milele na milele wasikuone.

Si unaona bastola hii. Ina kiwambo cha kuzuia sauti. Si kama hiyo ya kwako. Ingewashtua hata waliolala saa hizi. Hii unakufa kimyakimya na usiku huu huu unatumbukizwa kwenye buti ya gari, bahariniii... ukawe msosi wa samaki."

"Hallow Chiko mi n'shachoka bwana, hebu maliza kazi, mmalize tu.

Ghafla taa zilizimika. Wakati huo huo, milio miwili mikali ya risasi ilisikika masikioni mwa Donald. Kitendo bila kuchelewa, alibiringita hadi kwenye pembe ya chumba hicho kwa nia ya kukwepa risasi.




**Alijua kabisa ilikuwa kazi iliyofanywa kwa ufanisi na Inspekta Andrew. Akakumbuka alivyoamriwa na Inspekta huyo kuwaambia sehemu anayokwenda ili iwe rahisi kupata ulinzi, kuliko kujiendea mwenyewe kwani hivi sasa anaonekana anasakwa na watu kwa ajili ya kupoteza ushahidi wa mauaji wa Tausi.**

Kitu ambacho aligundua ni kwamba si taa za kwenye ukumbi wa kulia chakula pekee ambazo zilizimika, bali jengo zima. Hakuelewa kwa nini. Milio miwili ya risasi aliyoisikia, alidhani kuwa ilikusudiwa kumuua yeye na ilitoka kwenye bastola la Chiko.

Ni Chiko huyu huyu ambaye dakika moja tu iliyopita alimwambia kuwa bastola yake ina kiwango cha kuzuia sauti. Kwa mbali alisikia kama kelele na miguno ya maumivu.

Wakati akiwa amejikunja akiwaza mengi. Akiwaza nini cha kufanya kwani alitarajia zikamiminwa risasi zingine kwenye mwili wake, baada ya milio miwili ya risasi zilizoonekana kumkosa, ghafla tena taa ziliwashwa.

Watu watatu waliovalia kiraia waliingia. Donald aliyekuwa amejikunyata pembeni ya kabati, kwa macho yake alishuhudia watu wawili wakienda walipokuwa wameanguka Chiko na Doroth. Alichoshuhudia ni kwamba Chiko na mpenzi wake Doroth ambao walikuwa wakitamba dakika chache zilizopita, wakiwa kwenye harakati za kutaka kumuua wakiwa chini. Damu zilitapakaa kwenye chumba.

Kilichoonekana ni kwamba Chiko alikuwa amepigwa risasi mbili, mmoja mkononi na nyingine mguuni.

Mmoja alimfuata Chiko na kumvisha pingu haraka, mwingine akamfuata Doroth naye akapigwa pingu. Doroth alionekana hakufanya kitu chochote. Inavyoonekana kitendo cha taa kuzimwa ghafla na milio miwili ya risasi ilimtia kiwewe.

"Vipi hakuna lolote baya lililokutokea?" Ilikuwa na sauti ya mtu ambaye alibaki mlangoni. Kwa Donald ilikuwa kama sauti ya mtu anayemfahamu, lakini hakumbuki alionana naye wapi na walikuwa wakiongea wapi.

"Donald nakuuliza wewe?" Iliuliza tena.

Woga kidogo ulimwondoka Donald na kuangaza macho yake sawa sawa. Alimkumbuka. Alishawahi kumuona. Ni mmoja wa askari waliokuwa wakimlinda kwenye Hospitali ya Mwananyamala. Ilimshangaza kidogo kwa sababu hakuambiwa kuwa askari yule na mwenzake waliokuwa wakimlinda, watakwenda pale.

Alijua kabisa ilikuwa kazi iliyofanywa kwa ufanisi na Inspekta Andrew. Akakumbuka alivyoamriwa na Inspekta huyo kuwaambia sehemu anayokwenda ili iwe rahisi kupata ulinzi, kuliko kujiendea mwenyewe kwani hivi sasa anaonekana anasakwa na watu kwa ajili ya kupoteza ushahidi wa mauaji wa Tausi.

Akakumbuka maongezi yake na Inspekta Andrew wakati akitaka kutoka kwenye Hospitali ya Mwananyamala.

"Afande mimi nimeshapewa ruhusa hapa. Lakini hawa maafande wanaonilinda hapa wamesema hawawezi kuniruhusu mpaka wewe uamuru." Ilikuwa sauti ya Donald ambaye alikuwa bado kwenye Hospitali ya Mwananyamala, akiguza majeraha ya ajali aliyoipata.

"Kwani unataka kwenda wapi?"

"Nyumbani Inspekta, unataka nikae hapa milele?"

"Hapana, nilikuwa nasema hivyo kutokana na usalama wako. Kumbuka kuwa hao askari wamekaa hapo kwa ajili ya kukulinda. Ni wewe mwenyewe ulisema kuna watu wanakufuatilia."

"Ndiyo ni kweli, lakini nilikuwa nahitaji kuondoka hapa ili nikafanye mipango mingine. Kumbuka afande hata mimi nalazimika kutafuta ushahidi mwingine. Huo mlio nao ni mimi ndiye niliyewapa. Na hapa kuna kitu nafuatilia, inawezekana kabisa nikapata mwingine na kukurahisishieni kazi." Yakaja mazungumzo ya dakika 15 ambayo mwanzo hayakuwekwa. Nayo ni haya hapa.

"Ninachotaka hapa ni kwamba kabla ya kuondoka, nijue unakwenda wapi na unakwenda kufanya nini?" "Inspekta nakwenda nyumbani, lakini majira ya usiku nakwenda nyumbani kwa dada mmoja anaitwa Doroth, nyumba namba 78 maeneo ya Namanga."

Jina la Doroth lilimfanya Inspekta Andrew kushtuka. Akakumbuka kuwa ni mwanamke ambaye alikuwa mmoja wa namba zake za simu zilikuwa zikiwasiliana na namba za Peterson Donald na Bogota, kwa ajili ya kumuwinda Tausi. Ndipo Inspekta alipomwambia Donald ampe simu mmoja wa askari waliokuwa wodini na kumwambia:

"Kama amesharuhusiwa, basi na nyinyi ondokeni, mwacheni aende zake. Lile tishio la usalama wake sasa halipo," aliamuru.

Baada ya dakika kadhaa aliwapigia na kuwaambia wamfuatilie Donald bila yeye kujua kwa sababu anakwenda sehemu ambayo anahisi ni ya hatari au inaweza kuwafanya kuwa karibu kumpata muuaji wa Tausi.

Wakati askari wale waliokuwa wakimlinda hospitalini wakimfuata kwa uangalifu, waliongezewa mtu mwingine ndipo safari ya kumfuatilia iliwapeleka hadi Namanga na kukutana na mkasa huo.

**INAENDELEA JUMAPILI**



# IRENE ATAMBA KUVUKA MIPAKA KUTANGAZA INJILI

BAADA ya mashabiki kupokea vizuri wimbo wake mpya unaoitwa mabilioni, msanii wa muziki wa Injili, Irene Robert, amesema ana mpango wa kufanya kolabo na wanamuziki wakubwa Afrika.

Akizungumza na BT jana, Irene amesema wimbo wake huo ambao amemshirikisha msanii kutoka nchini DRC, unafanya vizuri na inaonyesha jinsi gani mashabiki wanapenda kuendelea na moto huo.

"Nimefurahi kuona wimbo wangu Mabilionea umepokelewa vizuri, nataka kuwahakikishia mashabiki wangu kwamba nitaendelea na mpango wa kuwashirikisha wasanii wengine wa Kiafrika katika huduma hii ya kumtukuza Mungu," amesema Irene

Irene ametoa nyimbo tofauti ikiwamo 'Nivushe' ambayo amemshirikisha msanii Angel Gadina kutoka Kenya na Sitalia aliyofanya na Christina Shusho.

## DIRECTOR P

# Mzambia anayetikisa Canada muziki wa Afrika

UKUAJI wa muziki wa Kiafrika katika nchi za ughaibuni unatokana na watu kujitoa katika kuusimamia na kueendeza, miongoni mwa watu hao ni Patrick Lupasa, maarufu kama Director P, ambaye makazi yake yapo nchini Canada.

Director P, ambaye ni Mzambia amekuwa na mchango mkubwa kwa wasanii wenye asili ya Afrika Mashariki wanaioshi nchini humo kwa kuwatengenezea muziki pamoja na kushiriki katika uimbaji.

Licha ya kazi ya uprodyuza, pia ni mwongozaji wa video katika studio anayoimiliki ya Lupasa Records.

Anasema aliondoka Zambia mwaka 2012 na kuhamia Canada, akifuata nyayo za babu yake ambaye alikuwa msanii wa uchekeshaji na baba yake ambaye alikuwa ni DJ.

"Nimekuwa nikitaka kuwa kwenye tasnia ya muziki lakini mwaka 2019 ndipo nilianza rasmi kisha kuanza kutoa muziki wangu mnamo 2020," amesema Director P.

**KOLABO**

Director P anasema mbali na wasanii wengi wa Afrika kutamani kufanya kazi na mastaa wakubwa kama Diamond Platnumz, Harmonize na wengineo, yeye anatamani kufanya kolabo na wasanii wenye majina ya wastani kama vile Swat Matire, Maandy, Kelechi Africana na Noti Flow.

Licha ya kuishi ughaibuni lakini msanii huyo aliyewahi kutamba na nyimbo kama Ninaamini Mama na Nionyeshe, bado analithamini na kulipenda soko la muziki wa Afrika.

**MIPANGO YAKE**

Director P anasema anatarajia kutembelea Tanzania mwaka ujao na kufanya kazi na wasanii wakubwa ili kujiongezea mashabiki na hivi karibuni ataachia wimbo wake mpya utakaotikisa chati mbalimbali za muziki.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### WATAJWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle huenda wakatumia hadi pauni milioni 190 kumpata mshambuliaji wa Tottenham na England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 28 na mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye miaka 22. ***(Telegraph)***

### CONTE AITAMANI NEWCASTLE

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Antonio Conte, anataka sana kuchukua nafasi ya Steve Bruce katika klabu ya Newcastle United. ***(Sun)***

### KUTUA ST JAMES' PARK

PHILIPPE Coutinho, 29, huenda akatua uwanja wa St James' Park kutoka Barcelona Januari 2022. ***(Sport)***

### RAPHINHA AVUTWA MAN UTD

KIUNGO wa Ureno, Bruno Fernandes, 27, amekuwa akiwasiliana na mchezaji nyota wa Leeds United, Raphinha, 24 raia wa Brazil, kuhusu uwezekano wa kuhamia Manchester United. ***(Mirror)***

### DEMBA ATAKA KURUDI

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Newcastle, Demba Ba,36, amejitolea kurejea tena kuichezea klabu hiyo baada ya kununuliwa. ***(Star)***

### RUDIGER ATAKIWA MADRID

MLINZI wa Ujerumani, Antonio Rudiger, 28, ni chaguo la kwanza la Real Madrid mwakani, mkataba wake wa sasa na Chelsea ukitarajiwa kukamilika msimu huu wa joto. ***(ABC, via Mail)***

### NYOTA KUONDOKA ARSENAL

NYOTA wa England, Ainsley Maitland-Niles, 24, na kiungo wa kati wa Misri, Mohamed Elneny mwenye umri wa miaka 29, huenda wakaondoka Arsenal Januari. ***(Sun)***

### DE BEEK ATAKIWA BARCA

BARCELONA wanamnyatia mchezaji wa kimataifa wa Uholanzi na klabu ya Manchester United, Donny van de Beek. ***(Sport)***

### AGUERO ALIIKATAA JUVE

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Sergio Aguero, 33, alikataa ombi la Juventus kutaka ajiunge nao kabla ya kwenda Barcelona kwa uhamisho huru, baada ya kuondoka Manchester City kipindi cha majira ya joto. ***(Sport)***

### RAMSEY KUUZWA JANUARI

JUVENTUS wanapanga kumuuza kiungo wa kati wa Wales, Aaron Ramsey, 30, Januari, huku West Ham na Everton zikionyesha nia ya kuwania saini yake. ***(Calcio Mercato)***

### ISCO AWANIWA LEICESTER

KLABU ya Leicester City wanapania kumsajili mchezaji nyota wa Real Madrid na Hispania, Isco mwenye umri wa miaka 29. ***(Fichajes)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LIONEL MESSI, JORGINHO WACHUANA BALLON D'OR

**Ni katika orodha ya wachezaji 30, EPL yatoa 10, Italia watano na..**

**PARIS,** Ufaransa

NYOTA wa Chelsea, Jorginho, fowadi wa Paris St-Germain, Lionel Messi na Robert Lewandowski wa Bayern Munich wametajwa katika orodha ya wanaowania tuzo ya mwanasoka bora wa mwaka, Ballon d'Or.

**Messi alishinda kwa mara ya sita mwaka 2019 na mwaka huu kwa mara ya kwanza alitwaa taji kubwa la kimataifa Copa America akiwa na kikosi cha Argentina.**

Kiungo wa Italia, Jorginho aliisaidia Chelsea kushinda taji la Ligi ya mabingwa Ulaya msimu uliopita, kabla ya kubeba Euro 2020.

Straika wa Poland, Lewandowski alishinda tuzo ya kiatu cha dhahabu msimu wa 2020-21, akiwa amefunga mabao 41 kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, wakati Bayern Munich ikitwaa taji la Ligi msimu uliopita.

Mshindi mara tano wa tuzo hiyo, fowadi wa Manchester United, Cristiano Ronaldo na kiungo wa Real Madrid, Luka Modric nao wametajwa kwenye kinyang'anyiro hicho.

Kuna wachezaji 14 wa Ligi Kuu England katika orodha hiyo ya wachezaji 30 na watano kutoka kikosi cha timu ya taifa ya Italia.

Tuzo ya Ballon d'Or, inaandaliwa na jarida la France Football, na inatolewa kila mwaka kwa mchezaji bora.

Tuzo hiyo haikutolewa mwaka 2020 kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1956 kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Tuzo hiyo itatolewa Novemba 29 jijini Paris nchini Ufaransa katika ukumbi wa Theatre du Chatelet.

Nyota wa England, Jude Bellingham (Borussia Dortmund), Mason Greenwood (Manchester United) na Bakayo Saka (Arsenal) ni miongoni mwa wachezaji 10 wanaowania tuzo ya Kopa Trophy, ambayo inatolewa kwa wachezaji chini ya umri wa miaka 21.

Kwenye tuzo ya golikipa bora maarufu kama Yashin Trophy wapo makipa wanne katika orodha ya watu 10 ambao ni Edouard Mendy wa Chelsea na Senegal, Ederson wa Manchester City na Brazil, Kasper Schmeichel wa Leicester City na Denmark na Emiliano Martinez wa Aston Villa na Argentina.

MECHI KALI
HOME
AWAY
BENIN
1.59 | 3.58 | 5.41
TANZANIA
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE KASINO

# TFF YATANGAZA UCHAGUZI UONGOZI BODI YA LIGI KUU

**Na Saada Akida**

KAMATI ya Uchanguzi ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) imetangaza uchaguzi mkuu wa Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu, Mkoani Kigoma.

**Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Uchanguzi wa TFF, Benjamini Kulume alisema kuwa kanuni ya TPBL, kifungu cha 29 inawapa ukomo viongozi walikuwapo madarakani kuendelea kuongoza.**

Alisema kanuni hiyo inawahitaji kuongoza kwa muda wa miaka minne ambayo tayari imeshatimia na kutakiwa kufanya uchaguzi kwa kugombea nafasi tano kwa mujibu wa kanuni ya bodi hiyo.

"Nafasi zinazogombewa ni Mwenyekiti (1), Makamu Mwenyeikiti (1), na kwa mujibu wa kanuni wanatakiwa kutoka klabu za ligi kuu, gharama za kuchukuwa fomu ni Sh. 200 000," alisema Kalume.

"Wajumbe wawakilishi wa klabu za ligi kuu nafasi tatu(3), wawakilishi wa klabu za ligi daraja la kwanza (2) na mtu mmoja kutoka klabu ya ligi daraja la pili na gharama zake za kuchukuwa fomu ni TZS 100,000," alisema Kalume.

Alisema fomu zitaanza kutolewa kesho (Jumatatu) Oktoba 11 hadi 15, saa 10 jioni na mwisho kuchukuwa na kurudisha fomu kwa wagombea ni Oktoba 16 na 17, mwaka huu na kutakuwa na kikao cha mchujo wa awali.

"Oktoba 20 hadi 22 mwaka huu ni kupindi cha kupokea na kuweka pingamizi kwa wagombea na tarehe 23 hadi 25 ni kusikiliza pingamizi na siku inayofuata ni usajili wa wagombea," alisema.

"Oktoba 30 hadi Novemba 2, Sekretarieti kuwasilisha masuala ya kimaadili kwa Kamati ya Maadili, Novemba 3 hadi 5, kipindi cha kupokea, kusikiliza na kutolea uamuzi masuala ya maadili."

Alisema Novemba 6 hadi 7 ni siku ya kutangaza matokeo ya uamuzi wa Kamati ya Maadili na tarehe 8 hadi 10, itakuwa kipindi cha kukata rufaa kwa uamuzi wa masuala ya kimaadili kwenye Kamati ya Rufaa ya TFF.

Kalume alisema siku inayofuata ambayo ni Novemba 11 hadi 13, watatoa uamuzi wa rufani, pia kutakuwa na kipindi cha kukata rufaa dhidi ya kamati ya uchanguzi kwenye kamati ya Rufani ya Uchanguzi ya TFF.

"Baaada ya michakato yote, Novemba 22 hadi 26, mwaka huu, ni kipindi cha kampeni kwa wagombea kwa ajili ya uchaguzi huo unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, huko Kigoma."



Mchezaji wa timu ya Mipango Veteran, Haji Zege (kushoto), akimpiga chenga mchezaji wa Ulinzi Veteran, katika mchezo wa kirafiki uliofanyika kwenye viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Jezi mpya za Kagera zawasili*

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE jezi mpya za klabu ya Kagera Sugar msimu wa 2021/22 zimewasili na zitaanza kuvaliwa rasmi kwenye mechi inayofuata ya Ligi Kuu kati ya timu hiyo dhidi ya Mbeya City, Oktoba 16 kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera.

Mtandao rasmi wa klabu hiyo umezichapisha jezi hizo kwenye mtandao wao wa kijamii, ukionyesha kuvaliwa na baadhi ya wachezaji wa klabu hiyo.

Kagera Sugar ilicheza mechi mbili, Septemba 29 dhidi ya Yanga na kuchapwa bao 1-0, pia Oktoba 3 dhidi ya Namungo na kutoka sare ya bao 1-1, bila ya kuwa na jezi mpya.

Mashabiki wengi waliokuwa wakitazama mechi kwenye televisheni, walionekana kushangazwa na jezi zilizotumiwa na timu hiyo, kutokana na kutokuwa na mwonekano mzuri, ubora hafifu, lakini zikiwa hazina hata nembo ya klabu hiyo.

Viongozi wa klabu hiyo walijitetea kuwa waliingiza jezi mapema, lakini kampuni moja ya nje ambayo walioiagiza ndiyo iliyochelewesha kuzileta hadi ligi ilipoanza, zilikuwa bado hazijatua nchini.

## HABARI MICHEZO

LIVE IN PLAY

SPORTPESA APP
BET LEO UWE MILIONEA
PAKUA SASA



# LAPORTA ATAKA KOEMAN AVUMILIWE

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA inajisikia fahari kuwa na kocha mkuu kama Ronald Koeman na anatakiwa kuaminiwa kama ilivyokuwa kwa Frank Rijkaard, amesema rais wa Klabu hiyo, Joan Laporta.

Kocha wa zamani wa Uholanzi, Koeman alionekana kuwa kwenye uwezekano wa kufukuzwa pale Barca wakati uvumi ulipoenea kuelekea kwenye mchezo dhidi ya Atletico Madrid Jumamosi iliyopita kuwa ndio unaweza kuwa mchezo wake wa mwisho.

Lakini Laporta amesisitiza Koeman anaweza kubakia klabuni hapo licha ya matokeo mabaya na kwamba anahitaji kuaminiwa.

Barcelona kwa sasa ipo nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga na inashika mkia kwenye kundi E kaika michuano ya Ligi ya mabingwa Ulaya, baada ya kufungwa na Bayern Munich na Benfica.

Na sasa Laporta amemkingia kifua Koeman na kutakiwa kuvumiliwa kama ilivyokuwa kwa Rijkaard, ambaye alitwaa taji la Ligi ya mabingwa Ulaya mwaka 2006.

Laporta ameelezea kuwa Koeman anakabiliwa na wakati mgumu hasa baada ya kuondoka kwa Lionel Messi, na matatizo ya kifedha yaliyoikumba klabu hiyo.

"Uamuzi ni kwamba, Koeman anaendelea," alisema Laporta akinukuliwa na RACI.




# Newcastle yamwania Icardi

**NEWCATLE,** England

BAADA ya kununuliwa kwa fedha ndefu, Newcastle United imeingia kwenye mbio za kuwania kumsajili fowadi wa Argentina, Mauro Icardi kutoka Paris Saint-Germain, kwa mujibu wa Calciomercato.

Newcastle inataka kufanya usajili mkubwa wakati wa dirisha dogo la Januari baada ya kuchukuliwa na mmiliki mpya.

Magpies hao wapo nafasi ya 19 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England, ikiwa haijashinda mchezo wowote na imetoka sare tatu kati ya mechi saba ilizocheza hadi sasa msimu huu.

Newcastle ilinunuliwa rasmi na serikali ya Saudi Arabia Alhamisi na sasa ni wamiliki rasmi wa klabu hiyo yenye maskani yake pale St James' Park.

Tottenham na Juventus ziliripotiwa kuwania kutaka kumsajili mchezaji huyo wa zamani wa Inter Milan, mwenye umri wa miaka 28, ambaye alijiunga na PSG kwa mkataba wa kudumu mwaka 2020 akisaini miaka minne kucheza hapo.

Gazeti la Telegraph limedai kwamba, Newcastle inaweza kutumia karibia pauni milioni 190 kwa usajili wa Januari na haitakuwa imevunja sheria ya haki na usawa wa ununuzi wa wachezaji.

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAPILI - 10 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3573 | Granada B vs Toledo | 1.81 | 3.14 | 4.44 |
| 13:00 | 4678 | Atletico Baleares vs CD Linares | 1.84 | 3.25 | 4.08 |
| 13:00 | 5968 | Socuellamos vs Real Murcia | 2.90 | 2.90 | 2.47 |
| 13:35 | 2622 | Belshina vs Slonim | 1.18 | 5.80 | 13.52 |
| 14:00 | 1866 | AB Gladsaxe vs Kolding IF | 2.50 | 3.47 | 2.46 |
| 15:00 | 2363 | Real Sociedad B vs Ponferradina | 2.41 | 3.06 | 3.01 |
| 15:00 | 3981 | Nigde Bld vs Afjet Afyonspor | 3.52 | 4.05 | 1.77 |
| 15:30 | 2032 | Sudtirol vs Giana Erminio | 1.68 | 3.56 | 5.14 |
| 15:30 | 2034 | Seregno Calcio vs Mantova | 2.47 | 3.20 | 2.95 |
| 15:30 | 2105 | Lucchese vs Vis Pesaro | 2.63 | 2.98 | 2.83 |
| 15:30 | 2533 | Albinoleffe vs Renate | 2.35 | 3.08 | 3.13 |
| 15:30 | 5682 | ADO Den Haag vs Den Bosch | 1.51 | 4.41 | 5.10 |
| 16:00 | 1298 | Italy vs Belgium | 2.26 | 3.39 | 3.19 |
| 16:00 | 3122 | Kenya vs Mali | 3.87 | 2.81 | 2.08 |
| 16:00 | 3346 | Hostoun vs Loko Vltavin | 4.07 | 4.17 | 1.64 |
| 16:00 | 3956 | CA Boston River vs CD Villa Espanola | 1.82 | 3.62 | 3.72 |
| 16:00 | 4071 | Uganda vs Rwanda | 1.58 | 3.35 | 6.03 |
| 16:00 | 4277 | Central African Republic vs Nigeria | 13.52 | 5.02 | 1.22 |
| 16:00 | 4382 | Covilha vs Nacional Madeira | 2.74 | 2.99 | 2.59 |
| 16:00 | 4455 | Thisted FC vs FA 2000 | 1.64 | 3.82 | 4.45 |
| 16:00 | 5050 | Sandecja vs Miedz Legnica | 3.11 | 3.06 | 2.24 |
| 17:00 | 1611 | Internacional vs Chapecoense | 1.46 | 3.96 | 6.38 |
| 17:00 | 1844 | Benin vs Tanzania | 1.59 | 3.58 | 5.41 |
| 17:00 | 4124 | Sollentuna Utd FF vs Sandvikens IF | 3.05 | 3.63 | 2.03 |
| 17:45 | 4178 | Dordrecht vs Helmond Sport | 2.89 | 3.42 | 2.24 |
| 18:00 | 2246 | Barcelona B vs FC Andorra | 2.33 | 3.11 | 2.91 |
| 18:00 | 2979 | CD Teruel vs CD Ebro | 1.75 | 3.25 | 4.66 |
| 18:00 | 3363 | Villarreal B vs Sevilla Atletico | 1.62 | 3.72 | 4.74 |
| 18:00 | 4293 | Racing Ferrol vs CD Badajoz | 3.05 | 3.20 | 2.20 |
| 18:30 | 1254 | Leixoes vs CD Feirense | 2.73 | 3.08 | 2.54 |
| 18:30 | 1888 | Palermo vs Foggia | 2.33 | 3.28 | 2.98 |
| 18:30 | 2746 | Catania vs Juve Stabia | 2.53 | 3.07 | 2.87 |
| 18:30 | 4506 | Monopoli vs Campobasso Calcio | 1.81 | 3.41 | 4.45 |
| 19:00 | 3182 | Merida UD vs CD Coria | 1.67 | 3.38 | 5.02 |
| 19:15 | 1084 | Alcorcon vs Burgos | 2.47 | 2.87 | 3.11 |
| 19:15 | 1633 | Fuenlabrada vs Leganes | 2.60 | 2.85 | 2.95 |
| 19:15 | 3948 | Tenerife vs Amorebieta | 1.59 | 3.50 | 6.31 |
| 19:30 | 2146 | Atletico Pulpileno vs Hercules CF | 2.77 | 2.96 | 2.52 |
| 20:00 | 2418 | La Serena vs Cobresal | 2.77 | 3.35 | 2.30 |
| 20:00 | 3800 | Zambia vs Equatorial Guinea | 1.65 | 3.54 | 4.85 |
| 20:00 | 4497 | Zacatepec vs CF Atlante | 2.26 | 3.25 | 2.91 |
| 20:00 | 5849 | Madagascar vs DR Congo | 3.88 | 2.81 | 2.08 |
| 21:00 | 1265 | GD Chaves vs Penafiel | 2.07 | 3.23 | 3.42 |
| 21:00 | 4475 | Almere City vs De Graafschap | 2.64 | 3.62 | 2.32 |
| 21:30 | 5089 | CF Estrela vs Viseu | 2.08 | 3.52 | 3.13 |
| 21:45 | 4240 | Spain vs France | 2.93 | 3.23 | 2.51 |
| 22:00 | 5170 | Santos vs Gremio | 2.67 | 2.96 | 2.62 |
| 23:00 | 5411 | Bolivia vs Peru | 2.90 | 3.35 | 2.40 |
| 23:00 | 5646 | Minnesota Utd vs Colorado Rapids | 2.26 | 3.45 | 3.05 |
| 23:30 | 4109 | Venezuela vs Ecuador | 4.00 | 3.10 | 2.05 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Oktoba 10, 2021

Nipashe




Newcastle yamuwania Icardi UKURASA 23

# STARS KUPINDUA MEZA LEO BENIN

## ●●● Twiga Stars yatwaa kombe la COSAFA, Tanzanite yaibutua Eritrea, sasa yasubiria...

**Na Adam Fungamwango**

IKIWA na kumbukumbu ya kufungwa bao 1-0 nyumbani, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Alhamisi iliyopita, timu ya taifa ya Tanzania, Taifa Stars, leo itakuwa ugenini ikijaribu kulipiza kisasi itakapovaana na Benin, mechi ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Dunia zinakazofanyika mwakani nchini Qatar.

**Mechi hiyo inatarajiwa kucheza jijini Cotonou, kwenye Uwanja wa L'Amitie nchini Benin, ambao una uwezo wa kuingiza wati 20,000.**

Itakuwa ni mechi ngumu kwa timu zote mbili kwa sababu baada ya kucheza mechi ya kwanza na kukaa kwa siku mbili tu, tayari makocha wa timu zote wanaonekana tayari wameshajuana mbinu na kila mmoja kumsoma mwenzake.

Kocha Mkuu wa Stars, Kim Poulsen, amesema Tanzania ina uwezo wa kushinda mechi hiyo, iwapo wachezaji watacheza kama walivyofanya kwenye mechi ya kwanza, hasa kipindi cha pili.

"Kipindi cha pili tuliwashambulia sana, ila walikuwa wamerudi nyuma, na walivyopata bao waliamua kulinda, lakini natumaini kwao watacheza kwa kufunguka wakisaka ushindi, hii inaweza kuwa nafasi ya wachezaji wetu tutengeneza nafasi nyingi na zikitumiwa vizuri, basi tunaweza kupata matokeo mazuri," alisema.

Timu zote zitakuwa zinasaka ushindi kwa udi na uvumba, kwani sare yoyote inaweza kuzifanya timu hizo kujiweka kwenye mazingira mabaya ya kumaliza mechi ikiwa juu Kundi J.

Stars ambayo inashika nafasi ya tatu kwa pointi nne inahitaji ushindi ili ifikishe pointi saba na kuzidi kuikaba koo Benin kileleni, lakini wenyeji wao wenye pointi saba na wanaoongoza kundi, wanahitaji pia ushindi ili ifikishe pointi 10 na kuikimbia Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo ambayo hata kama ikiifunga Madagascar itakuwa imefikisha pointi nane.

Ikumbukwe kuwa ni mshindi mmoja tu kwa kila kundi kuanzia A hadi J, ndiyo watakaosonga mbele kwenda kwenye hatua za mtoano, kabla ya kupata tano tu zitakazoiwakilisha Afrika kwenye michuano hiyo.

**Wakati huohuo**, timu ya taifa ya wanawake ya Tanzania, Twiga Stars, imefanikiwa kutwaa Kombe la COSAFA baada ya kuichapa timu ya taifa ya Malawi bao 1-0 kwenye fainali ya michuano hiyo, inayozishirikisha timu ya taifa za Ukanda Kusini mwa Afrika.

Tanzania ambayo ilikuwa mgeni mwalikwa kwenye michuano hiyo iliyofanyika nchini Afrika Kusini, ilipata bao pekee kwenye Uwanja wa Nelson Mandela Bay, Port Elizabeth, dakika ya 65 lililowekwa kwenye kamba na beki wa kushoto, Enekia Kasonga.

Mchezaji huyo aliutokea mpira uliotemwa na kipa wa Malawi, Lucy Mhango, uliotokana na faulo iliyopigwa na Fatuma Selemani, baada ya Olpa Clement kuangushwa nje kidogo ya eneo la hatari.

Nayo, timu ya taifa ya Tanzania wanawake chini ya miaka 20, imefanikiwa kusonga mbele kwenye kinyang'anyiro cha kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Dunia nchini Costa Rica mwakani baada ya kuichapa Eritrea mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Yalikuwa ni mabao ya Irene Kisisa dakika ya 55 na Protas Mbunda dakika ya 84, yaliyotosha kuifanya Tanzanite kuibuka na ushindi huo.

Kwa matokeo hayo, Tanzania imesonga mbele kwa jumla ya ma bao 5-0, kwani kwenye mechi ya kwanza ugenini, Septemba 25, ilishinda mabao 3-0.



Nahodha wa timu ya Twiga Stars, Amina Bilali, akimtoka mchezaji wa Malawi wakati wa mchezo wa fainali ya kombe la COSAFA 2021 baina ya timu hizo, uliopigwa uwanja wa Nelson Mandela Bay jijini Johannesburg, Afrika Kusini. Twiga ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDANO**

## Nabi asuka upya safu ya ushambuliaji

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, amesema wako makini kuzitumia vyema siku za mapumziko ya kalenda ya Fifa kuhakikisha wanatengeneza muunganiko mzuri, utulivu na umakini kwenye safu ya ushambuliaji.

Nabi ameiamulia safu ya ushambuliaji ya Yanga kwa sasa inaongozwa na Fiston Mayele, Heritier Makambo na Yusuph Athumani kuhakikisha wanakuwa makini na kuipatia idadi ya mabao mengi kwa kila mechi ilizopo mbele yao.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Nabi alisema katika michezo miwili ya ligi waliocheza ameona udhaifu wao ikiwemo washambuliaji kushindwa kutumia vema nafasi wanazotengeneza pamoja na kucheza kipindi kimoja na kukosa ufiti.

Alisema siku za mapumziko ya kalenda ya Fifa, wamezitumia kama matarajio yake na wanaendelea kufanyia kazi makosa yao na kuhakikisha wanakuwa imara na kuendelea na kasi yao ya ushindi watakaporejea katika ligi hiyo.

"Hizo mechi mbili tumepata ushindi na kukusanya pointi sita, licha ya kuendelea kuimarika baadhi ya nafasi, lakini tatizo liko kwenye ushambuliaji kwa kutengeneza nafasi nyingi, lakini kutokuwa na utulivu tunashindwa kutumia na kupata idadi ya mabao mengi,".

"Nafanyia kazi makosa hayo madogo madogo, tutakaporejea katika mechi zetu za ligi tuwe tunashinda idadi ya mabao mengi ikiwemo mbili na kuendelea, morali ya wachezaji ipo jambo na tunamatarajio ya kufanya vizuri msimu huu," alisema Nabi.

Alisema malengo yao makubwa ni kupata ushindi wa mabao mengi katika kila mchezo ili kufikia malengo yao ya kuhakikisha msimu huu wanatwaa ubingwa wa Ligi Kuu.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >